Strategic Initiative for Women in the Horn of Africa | SIHA Network

Women's International Peace Centre — Amplifying Women's Voice and Power

KUJITAYARISHA NA KUSHUGHULIKIA VISA VYA UNYANYASAJI WA KIJINSIA WAKATI WA DHARURA

NAFASI ZA KUTUMIA LUGHA INAYOLETA MABADILIKO KATIKA MITAZAMO YA UFEMINISTI KWA UBIA

Zawadi ya Serikali ya Marekani

Ilitungwa 2020

SHUKRANI

IRC ingependa kuwashukuru wanawake na wasichana mbalimbali, wanaharakati wa haki za wanawake, mashirika, mitandao na watendaji wa kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia (GBV) ambao wamechangia katika maandalizi ya ripoti hii. Ripoti hii iliandaliwa kupitia ushirikiano kati ya: Akina Mama wa Afrika, GBV Prevention Network, Gender Equality Network - Myanmar, Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji (IRC), El-Karama, Strategic Initiative for Women in the Horn of Africa na Women's International Peace Centre.[1]

Shirika la IRC linatambua kazi muhimu iliyofanywa na Dr. Michelle Lokot, aliyeongoza juhudi za kuandaa utafiti huu.

IRC inashukuru Ofisi ya Kuhesabu Watu, Wakimbizi na Uhamiaji - Idara ya Majimbo ya Marekani[2] kwa kufadhili muungano wa Building Local Thinking Global (BLTG) tangu 2017, kama zawadi ya Serikali ya Marekani.

1 Akina Mama wa Afrika: https://www.akinamamawaafrika.org; GBV Prevention Network: https://preventgbvafrica.org; Gender Equality Network – Myanmar: https://www.genmyanmar.org; El-Karama: https://www.elkara.ma; Strategic Initiative for Women in the Horn of Africa: https://sihanet.org; Women's International Peace Centre: https://wipc.org.

2 https://www.state.gov/about-us-bureau-of-population-refugees-and-migration/

YALIYOMO

UFUPISHO **4**

Usuli 6

Maswali muhimu 7

Methodolojia 7

Uchanganuzi wa matini na dhana kuu 8

Fikra za kifeministi 10

MATOKEO **12**

Maneno ya kawaida na safu zake za mamlaka 12

Lugha na utambulisho 19

Lugha na kufumba macho 19

Uhusiano kati ya lugha, mamlaka na njia za kufanya kazi 20

Lugha na mienendo badilifu ya "nchini" na "kimataifa" 21

Urithi wa kikoloni na ubaguzi wa rangi, ulioimarishwa na lugha ya misaada 23

HATUA ZA KUCHUKUA: KUBUNI LUGHA MPYA **24**

Maadili na njia za kufanya kazi 25

Mapendekezo 28

UFUPISHO

Kwa njia nyingi, maneno tunayotumia hubuni ukweli tunaoona. Maneno yanaweza kuwasiliana upendeleo na historia yetu, na kuathiri jinsi tunavyoona mazingira yetu na watu ambao tunashirikiana nao. Kwa miaka kadhaa, muungano wa Building Local Thinking Global (BLTG) - kikundi cha mitandao ya haki za wanawake na mashirika wanachama kutoka Asia, Afrika Mashariki na Mashariki ya Kati - umejadili jinsi safu za mamlaka zinavyoundwa na kuimarishwa na lugha inayotumiwa katika sekta ya kibinadamu. Ripoti hii, iliyo andaliwa kwa kushauriana na wanachama wa BLTG unalenga kuchunguza lugha na safu za mamlaka katika misaada ya kibinadamu, na athari za lugha kwa uhusiano kati ya vikundi tofauti. Lengo lake ni kutambua lugha mpya ambayo inajumuisha na kuwezesha, na inaendeleza usawa.

Katika utafiti uliotumika kuandaa ripoti hii, wahojiwa walitambua kiwango chao cha kuridhishwa na maneno yanayotumiwa sana katika sekta ya kibinadamu. Maneno matano yanayoongoza yasiyoridhisha kuelezea watu binafsi, vikundi au mashirika yalikuwa: mwathiriwa (victim), za kipato cha chini (third world), waliotengwa (marginalized), wachache (minority) na kuathirika kwa haraka (vulnerable). Wakati wa mahojiano na majadiliano ya vikundi, washiriki walijadili maneno haya na mengine kwa undani zaidi, wakionyesha safu nyingi za mamlaka ambazo zinachangia katika uelewa wa maneno fulani na ambazo zinaendelezwa na matumizi ya maneno fulani. Washiriki wajadili jinsi lugha inaweza kufanya watu wajihisi wamejumuishwa au wametengwa, wanaonekana au wanapuuzwa. Walisema kuwa mashirika ya nchini mara nyingi hulazimika kutumia istilahi fulani ambazo yanashinikizwa kutumia ili kupata ufadhili.

> *Lugha ina nguvu. Maneno tunayotumia huwa sehemu ya ufahamu wetu. Tunapoyatumia tena na tena, maneno haya yanakuwa ya kawaida.*
>
> Mhojiwa, Mashariki ya Kati

Si jambo la kushangaza kuwa majadiliano pia yalivuka mipaka ya lugha na kushughulikia mienendo badilifu ya mamlaka kati ya mashirika ya nchini na ya kimataifa na pia kati ya mashirika ya nchini na wafadhili. Washiriki walionyesha jinsi mienendo badilifu isiyo sawa ya mamlaka na ufikiaji wa rasilimali husababisha kutofautiana katika mishahara na mikataba. Pia waliongeza kuwa michakato ya uongozi kutoka juu kurudi chini wanayolazimika kufuata mara nyingi hailingani na kile wanachojua au kile jamii zinataka.

Katika ripoti hii, mara kwa mara tunatumia neno "shirika la nchini" kuonyesha jinsi washiriki walijadili neno hili na vile vile jinsi lugha hii inavyoonekana katika matini, hasa matini kuhusu ujanibishaji. Majadiliano kamili ya matumizi ya "Ya nchini" yanaweza kupatikana kwenye kurasa za 21-22

Kulingana na matokeo hayo, mapendekezo kadhaa muhimu yaliibuka ili kuwezesha lugha inayojumuisha na inayowezesha zaidi. Tunahisi hatua hii pia itakuza ubia wa kifeministi wenye usawa zaidi miongoni mwa aina tofauti za wahusika kwenye miktadha ya kibinadamu. Zifuatazo ni hatua ambazo watendaji wa kibinadamu wanapaswa kuchukua.

CHAGUO ZA LUGHA:

- Uliza jamii ni maneno yapi wangependa yatumike kuwaelezea.
- Tambua fursa za wahusika wenyeji kuongoza katika kukuza istilahi kulingana na maarifa yao ya muktadha, ukitambua kuwa kufanya hivi kunamaanisha kuwa huenda watendaji wa kimataifa na wafadhili wakahitaji kutafakari juu ya jinsi wanavyotumia mamlaka yao kuathiri istilahi na kutafuta namna ya kushiriki mamlaka yao.
- Tambua kuwa maneno yana maana tofauti kulingana na muktadha na hakuna uwezekano kwamba maneno yatafaa miktadha na lugha zote.
- Tambua maneno yanayofaa na yanayoambatana na muktadha, ambayo yanaeleweka katika lugha za wenyeji, yanayoweza kutumiwa kama vibadala panapohitajika.
- Hakikisha kuwa kubadilisha maneno ili kuyafanya yawe jumuishi na yawafae wenyeji hufanywa kwa kuchambua na kutambua mamlaka, na sio tu kwa ajili ya kufumba macho au kutumika tu kulainisha au kuepuka mitazamo ya mamlaka.

LUGHA NA MAMLAKA:

- Buni fursa za kushawishi watendaji wengine wa kibinadamu kukuza istilahi inayojumuisha na kuwezesha zaidi kulingana na mapendekezo kutoka kwa jamii na watu wanaoufahamu muktadha.
- Fafanua wazi maana ya maneno muhimu ambayo hutumiwa katika sekta ya kibinadamu, kwa kuzingatia mienendo badilifu ya mamlaka inayoambatana na baadhi ya maneno, kutokuwepo kwa lugha fulani ya kiufundi na athari za maneno kama haya kwa vikundi tofauti.
- Tafakari kwa kina na utambue sehemu ambazo ukosefu wa usawa kimamlaka huathiri uhusiano kati ya mashirika ya nchini na ya kimataifa, na kati ya mashirika ya nchini na wafadhili.

LUGHA KATIKA UBIA:

- Kimakusudi, anzisha ubia sawa ili ushirikiano usijikite tu katika kutumia mashirika ya "nchini" kama washirika wanaotekeleza, lakini badala yake ushughulikie kwa busara safu za mamlaka kati ya wahusika tofauti katika kila hatua ya ushirikiano.
- Zingatia fadhili na huruma katika kuanzisha na kudumisha ubia na wahusika tofauti wa kibinadamu, huku ukichukua muda na kuwa mwangalifu ili kuhakikisha uhusiano wowote ni wa heshima, unajumuisha, unawezesha na unaongozwa na kanuni ya kugawana mamlaka.

Aidha, washiriki walipendekeza mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kufikiria kuhusu istilahi za kutumia. Mapendekezo haya mbadala ya lugha ya kuzingatiwa yanapatikana kwenye ukurasa wa 26-27. Kwa pamoja, matokeo, mapendekezo na istilahi mbadala zinatoa njia ya kusonga mbele katika kutambua nguvu ya lugha na jinsi tunaweza kutumia lugha kugeuza mamlaka.

USULI

Kwa njia nyingi, maneno tunayotumia hubuni ukweli tunaoona. Maneno yanaweza kuwasiliana upendeleo na historia yetu, na kuathiri jinsi tunavyoona mazingira yetu na watu ambao tunashirikiana nao. Kwa miaka kadhaa, muungano wa Building Local Thinking Global (BLTG) - kikundi cha mitandao ya haki za wanawake na mashirika wanachama kutoka Asia, Afrika Mashariki na Mashariki ya Kati - umejadili jinsi safu za mamlaka zinavyoundwa na kuimarishwa na lugha inayotumiwa katika sekta ya kibinadamu. Maneno kama "kutengwa," "mnufaishwa," na "kuathirika kwa haraka" huonyesha maisha ya jamii kwa njia isiyobadilika na isiyo na msaada, na yanaweza kuzidisha safu za mamlaka zisizo sawa kati ya mashirika ya kibinadamu na jamii. Lebo kama vile "shirika la nchini" na "shirika la kimataifa" pia huendeleza safu za mamlaka kati ya aina tofauti za watendaji wa kibinadamu.[3]

Muungano wa BLTG ulitambua haja ya ripoti inayojadili chaguo za lugha zinazotumiwa na mashirika ya kimataifa, hasa jinsi ambavyo lugha inaweza kuendeleza upendeleo na safu za mamlaka. Kupitia ripoti hii, tunajaribu kuchunguza jinsi fikra za kifeministi zinaweza kutoa fursa kwa lugha inayojumuisha na kuwezesha, na pia ushirikiano sawa wa kifeministi.

Ripoti hii imeandaliwa kupitia uchanganuzi wa matini, utafiti wa mtandaoni na wahojiwa 35, majadiliano ya vikundi na wanawake 19 na mahojiano ya kibinafsi na wanawake 10 wanaofanya kazi katika BLTG. Mtafiti wa nje aliongoza mchakato huu na kisha akafanya kikao cha uthibitishaji na wanawake 24. Matokeo ya kazi hii ni uchambuzi wa jinsi ambavyo maneno yanayotumiwa kwa kawaida katika kazi ya kibinadamu huonekana katika miktadha mbalimbali, nguvu za maneno haya na mapendekezo ya jinsi tutakavyosonga mbele kwa uelewa na uangalifu wa kina zaidi.

Ni muhimu kutambua kwamba ripoti hii, ambayo siyo tu pekee inayotambua mienendo ya lugha na mamlaka, inatokana kwa sehemu fulani na mazungumzo ya mapema ndani ya muungano wa BLTG ambayo yalikosoa jina letu kama kikundi. Building Local Thinking Global, jina la mradi lililochaguliwa wakati wa kubuniwa, linadokeza mienendo badilifu ya mamlaka isiyo na usawa, ambayo tunakosoa kama kikundi. Tulitaka kuchunguza kwa kina hasa jinsi chaguo za lugha zinaweza kuathiri usawa na haki, na kuwanyima watu, watendaji na jamii zingine nguvu. Ripoti hii inatoa mapendekezo kuhusu jinsi watendaji wa kibinadamu wanaweza kuchunguza lugha wanayotumia, jinsi inaendeleza upendeleo na ukosefu wa usawa wa kimamlaka, na hasa jinsi fikra za kifeministi zinaweza kusababisha kuanza kutumika kwa lugha inayoleta usawa wa kimamlaka na heshima.

Muungano wa BLTG[4] unaleta pamoja mashirika ya kutetea haki za wanawake, wanaharakati, wasomi, mashirika ya kijamii, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), na mitandao ya kijamii ya maeneo mbalimbali kwa lengo la kuungana kwa pamoja katika jamii ya kibinadamu kuhakikisha wanawake na wasichana wanalindwa dhidi ya GBV katika miktadha ya dharura. Mpango huo unaleta pamoja muungano wa mitandao ya haki za wanawake na mashirika wanachama kutoka Asia, Afrika Mashariki na Mashariki ya Kati.

[3] Katika ripoti hii, mara kwa mara tunatumia neno "shirika la nchini" kuonyesha jinsi washiriki walijadili neno hili na vile vile jinsi lugha hii inavyoonekana katika matini, hasa matini kuhusu ujanibishaji. Majadiliano kamili ya matumizi ya "Ya nchini" yanaweza kupatikana kwenye kurasa za 21-22

[4] Kwa pamoja, wanachama wa muungano wa BLTG wanahusika katika mpango wa kimataifa, unaohusisha mashirika mengi, ambao unakusudia kukuza uongozi unaoleta mabadiliko kwa wanawake katika kujitayarisha na visa vya Unyanyasaji wa Kijinsia wakati wa dharura. Muungano huo unajumuisha wafeministi, watetezi wa haki za wanawake, mashirika ya mashinani, wanaharakati, na mashirika ya kitaifa, ya kikanda, na mengine yanayoshirikiana, yanayofanya kazi katika hali zenye dharura na miktadha inayohitaji uangalifu, yaliyojitolea kulinda na kuwezesha wanawake na wasichana. Habari zaidi kuhusu mpango wa BLTG zinapatikana katika https://gbvresponders.org/building-local-thinking-global/.

MASWALI MUHIMU

Ripoti hii inajaribu kuchunguza lugha na safu za mamlaka katika miktadha ya misaada ya kibinadamu, na athari za lugha kwenye uhusiano kati ya vikundi mbalimbali, kwa lengo la kutambua lugha mpya inayojumuisha na inayowezesha, na kuendeleza usawa. Ripoti hii imejikita katika kutambua kwamba mamlaka na lugha zinategemeana na kuimarishana. Ili kuelewa jinsi mamlaka yanavyofanya kazi, lazima tuelewe athari za chaguo za lugha, zilizowekwa hasa katika safu tofauti za mamlaka ambazo huenda zinapatikana katika miktadha ya kibinadamu. Mamlaka hayaegemei upande mmoja; hayafanyi kazi tu kati ya watendaji wa kimataifa na wa nchini, lakini katika uhusiano wowote kwa wanawake na wasichana na kati ya watendaji walio nchini pia.

> *Lugha inaweza kutumika kama chombo, inaweza kutumika kama silaha, inaweza kutumika kama ngao. Ni muhimu sana ikiwa tunafanya kazi hii iliyojaa siasa, lugha ni muhimu sana na ni muhimu kutilia lugha maanani.*
>
> Mhojiwa, Afrika Mashariki

Ripoti hii pia inatambua kuwa hata lugha ambayo hapo awali ilikuwa inaendeleza haki na usawa wa jinsia inaweza kupoteza sifa hizo kadri muda unavyopita. Kazi yetu inahitaji tafakari muhimu mara kwa mara, juu ya manufaa ya maneno na misamiati fulani. Katika muktadha wa kuzuia na kukabiliana na GBV, ni muhimu kufikiria kwa makini kuhusu jinsi tunavyoelezea jamii katika dharura za kibinadamu na pia shughuli tunazobuni na kutekeleza.

Maswali muhimu ambayo ripoti hii inachunguza ni:

- Ni maneno au misemo gani inayotumiwa sana katika kazi ya kibinadamu inayoweza kuathiri mienendo badilifu ya mamlaka?
- Ni mienendo ipi badilifu ya mamlaka (ikiwemo madaraja ya mamlaka yanayotangamana, utambulisho na ubaguzi) inayohusishwa na lugha inayotumika sana wakati wa kutoa misaada ya kibinadamu?
- Je, lugha hiyo inaathiri vipi uhusiano kati ya wahusika tofauti wanaofanya kazi ya kuzuia na kukabiliana na GBV, kati ya watendaji hawa na umma au wafadhili, na kati ya watendaji hawa na jamii na wanawake na wasichana wanaowahudumia katika mazingira ya kibinadamu?
- Ni fursa zipi zinaweza kuwepo kwa fikra za kifeministi kutoa lugha mpya inayojumuisha na inayowezesha, na zinazokuza usawa katika ubia wa kifeministi na shughuli za kuzuia na kukabiliana na GBV?

METHODOLOJIA

Mbinu zilizotumiwa kuandaa ripoti hii ni pamoja na: uchanganuzi wa matini, utafiti wa mtandaoni, mahojiano yaliyokuwa na mpangilio kiasi, majadiliano ya vikundi (FGDs) na kikao cha uthibitishaji. Kazi hii iliongozwa na mshauri.

Uchanganuzi wa matini ulijumuisha matini za kitaaluma na ripoti za mashirika Yasiyo ya Kiserikali zinazojadili lugha, istilahi na safu za mamlaka katika sekta ya kibinadamu. Uchanganuzi wa matini ulisaidia katika kubuni muundo wa utafiti wa mtandaoni na miongozo ya majadiliano ya vikundi.

Utafiti wa mtandaoni ulifanyika katika kipindi cha wiki tatu, kutoka mapema Novemba 2020 na ulihusisha wanachama wa muungano wa BLTG na washirika wengine. Ulishirikiwa kupitia programu ya Survey Monkey katika lugha nne: Kiingereza, Kiarabu, Kiburma na Kifaransa. Kwa jumla, watu 35 walishiriki kwenye utafiti (asilimia 77 walikuwa wanawake, asilimia 14 wanaume, na waliosalia walipendelea kutosema au kutojieleza). Kwa jumla, asilimia 43 ya washiriki walitoka Afrika Mashariki, asilimia 29 walitoka Mashariki ya Kati na asilimia 29 walitoka Asia. Kwa jumla, asilimia 83 walikuwa wanachama wa BLTG na asilimia 17 hawakuwa. Mashirika mengi yalijitambua kama ya kutetea haki za wanawake (asilimia 54), yakifuatwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (asilimia 23), mashirika ya kijamii (asilimia 11), mitandao ya kitaifa ya asasi za kiraia (asilimia 6), wanaharakati (asilimia 3) na mashirika ya msaada ya serikali (asilimia 3).

Mahojiano yaliyokuwa na mpangilio kiasi yalifanywa kwa Kiingereza kupitia simu ya video na washiriki 7 wa BLTG na Wajumbe 3 wa Kamati ya Uendeshaji ya BLTG[5] (wote walikuwa wanawake) katika maeneo matatu ya kijiografia ambayo BLTG inazingatia: Asia, Afrika Mashariki na Mashariki ya Kati. Mahojiano haya yalilenga kujadili baadhi ya maneno muhimu yaliyotajwa katika utafiti huo, na vile vile safu za mamlaka katika sekta ya kibinadamu. Majadiliano ya vikundi yalifanywa kwa Kiingereza kupitia simu ya video na vikundi vitatu vilivyopangwa pakubwa kwa eneo la kijiografia. Kwa jumla, wanawake 16 na wanaume 3 walishiriki katika majadiliano ya vikundi. Washiriki walijadili matokeo ya utafiti wa awali, wakizingatia uzuri na ubaya wa kutumia istilahi fulani na pia safu za mamlaka katika sekta ya kibinadamu. Data ya mahojiano na majadiliano ya vikundi iliorodheshwa kwa misingi ya mada kuu na ikalinganishwa na data ya utafiti.

Kikao cha uthibitishaji kilifanyika na wanawake 19 na wanaume 5 wakitumia simu ya video. Mshauri huyo aliwasilisha matokeo ya utafiti, mahojiano na majadiliano ya vikundi, na aliwaalika washiriki watoe maoni yao na wajadili matokeo. Walioshiriki katika mahojiano na katika majadiliano ya vikundi pia walialikwa watoe maoni yaliyoandikwa kuhusu rasimu ya ripoti. Wanachama wote wa BLTG, ikiwemo IRC, walialikwa watoe maoni yaliyoandikwa kuhusu slaidi za PowerPoint zilizotumiwa katika kikao cha uthibitishaji, na baadaye watoe maoni yaliyoandikwa kuhusu rasimu ya ripoti.

Haimaanishi kuwa matokeo ya mchakato huu yanawakilisha wote katika mtandao wa BLTG, tukizingatia idadi ndogo ya washiriki, hasa kutokana na janga la COVID-19. Ni muhimu kutambua kwamba utafiti haukulenga kuwawakilisha wote, ikizingatiwa idadi ndogo ya waliolengwa kuhojiwa. Hata hivyo, utafiti huu unasaidia kutoa muhtasari wa maswala muhimu ambayo yalijadiliwa kwa kina wakati wa mahojiano na majadiliano ya vikundi. Aidha, dhana na mada zilizojadiliwa katika matokeo haziwakilishi uchambuzi kamili wa maswala, ikizingatiwa muda mdogo wa mahojiano na majadiliano ya vikundi. Si dhana zote katika utafiti ambazo zingeweza kujadiliwa katika mahojiano na majadiliano ya vikundi; kwa hivyo, kwa maneno kadhaa ambayo hutumiwa kawaida katika sekta ya kibinadamu, matokeo yanayowasilishwa ni ya utafiti pekee.

[5] Wanachama wa Kamati ya Uendeshaji ya BLTG ni Akina Mama wa Afrika, GBV Prevention Network, Gender Equality Network – Myanmar, El-Karama, Strategic Initiative for Women in the Horn of Africa, na Women's International Peace Centre.

Washiriki pia walitafakari kwa upana zaidi kuhusu safu za mamlaka katika sekta ya kibinadamu, ikiwemo katika uhusiano wao na wafadhili na jamii, jambo ambalo lilikuwa nje ya mawanda ya ripoti hii na kwa hivyo halikujumuishwa. Ripoti hii rasmi inawakilisha sehemu muhimu ya kuanza kwa safari inayoendelea ya kujifunza na kutafakari, ambayo inaweza kuendelezwa katika tafiti, majadiliano na matumizi ya baadaye. Lengo la ripoti hii ni kuhamasisha tafakari muhimu kuhusu lugha na mamlaka katika sekta ya kibinadamu.

UCHANGANUZI WA MATINI NA DHANA KUU

ATHARI ZA LUGHA

Ndani ya matini zilizoko zinazochambua lugha inayotumika katika sekta za kibinadamu na maendeleo, lugha imetambuliwa kama njia yenye nguvu ya kuhamasisha watu, ufadhili na ajenda. Katika ripoti hii, tunapendekeza kwamba lugha na mamlaka katika misaada ya kibinadamu zinategemeana na zinaimarishana: lugha inaendelezwa na safu za mamlaka, na safu za mamlaka zinaendelezwa na lugha.

Tangu katikati ya miaka ya 2000, wafeministi na weledi wa maendeleo wamefikiria sana kuhusu lugha inayotumiwa katika sekta za kibinadamu na maendeleo, hasa kwa kuhusiana na maswala ya usawa wa kijinsia.[6] Uchambuzi huu unaonyesha kwamba baadhi ya istilahi na maneno ambayo huenda kijuujuu yakaonekana kama yanavipa vikundi fulani sauti na chaguo zaidi, yanaweza kuwa chombo kinachoendeleza safu kuu za mamlaka au ajenda, kama vile ulegezaji wa masoko.[7] Wasomi wanasema kwamba maneno yanayovuma kama "jinsia"[8] "Uwezeshaji" au "ushiriki," yanaweza kupoteza

[6] Cornwall, A. & Brock, K. "What do buzzwords do for development policy? A critical look at 'participation,' 'empowerment' and 'poverty reduction,'" *Third World Quarterly*, 26:7, 1043-1060 (2005) hereafter, Cornwall & Brock; Cornwall, A. "Buzzwords and fuzzwords: deconstructing development discourse," *Development in Practice*, 17:4-5, 471-484 (2007); Eyben, R. & Napier-Moore, R. "Choosing words with care? Shifting meanings of women's empowerment in international development," *Third World Quarterly*, 30:2, 285–300 (2009), hereafter, Eyben & Napier-Moore.

[7] Cornwall & Brock, 1046; Eyben & Napier-Moore, 294-295.

[8] Schnable, A., et al. "International Development buzzwords: understanding their use among donors, NGOs, and academics," *The Journal of Development Studies* (2020), hereafter, Schnable, et al.

umuhimu wake kadri muda unavyopita na mwishowe kuwa maneno "yaliyopoteza ubainifu wake" ambayo kwa upande mmoja yanarejelea kila kitu na kwa upande mwingine hayana maana.[9] Kwa njia hii, lugha inaweza kutumika kutoa uhalali wa ajenda au njia fulani.[10] Kwa mfano, neno "uwezeshaji" mara nyingi hulinganishwa na kuwapa wanawake na wasichana ujuzi na ustadi (kana kwamba kimsingi hawana), huku likipuuza safu za mamlaka zilizojikita kwenye ubaguzi wa rangi, ukoloni, mipaka ya kijinsia na vigezo vingine, zinazotangamana ambazo zinaathiri maisha yao.[11] Kwa kufanya hivyo, lugha pia inaweza kutumiwa kutafuta masuluhisho kwa shida changamano kama taasubi ya kiume kwa njia rahisi, na kwa wakati huo kuondolea athari za siasa yale waliyopitia watu.[12] Hata neno "unyanyasaji wa kijinsia" (GBV) wakati mwingine limeondolewa athari za siasa, na kuwacha kuonekana kama linaloendeshwa na safu za mamlaka yasiyo na usawa kati ya wanaume na wanawake, na kuanza kuonekana kama dhana inayolenga vurugu inayofanyika kutokana na utambulisho na majukumu tofauti ya kijinsia.[13]

Uchambuzi wa chimbuko la maneno yanayovuma katika sekta ya kibinadamu pia ulitambua jukumu la wafadhili katika kuendeleza dhana. Kwa kutumia nafasi zao za nguvu za kifedha, wafadhili wanaweza kuathiri ajenda za programu kwa kusisitiza lugha fulani.[14] Hata hivyo, lugha pia inaweza kuendelezwa na hafla au migogoro ya kimataifa na hata wasomi.[15]

Lugha inaweza kutumiwa kama njia ya kuwatenga watu, hivyo kubuni "washiriki wa ndani" wa wataalamu wanaotumia lugha maalum.[16] Zana, miongozo ya matumizi na hata ya kiufundi inaweza kuwa na lugha inayopendelea ufundi zaidi ya uzoefu, na kusababisha aina fulani za maarifa kuthaminiwa kuliko zingine.[17] Ni muhimu kutambua kwamba dhana inayochukulia kuwa maarifa na mamlaka yanaongozwa na "Magharibi" inahitaji marekebisho; kuna ongezeko la kutambua kwamba maarifa ya "nchini" yanaweza pia kuimarisha maoni haya makuu yanayotambuliwa na wengi.[18]

Lugha pia inaweza kubagua. Kwa mfano, sauti za wanawake na wasichana zinaweza kurahisishwa na kufupishwa, hivyo kupuuza uzoefu wao na kuufanya wa jumla ili kuonyesha uhusiano na hitaji la ufadhili au shughuli ya programu.[19] Jambo hili linapotokea, watafiti na mashirika yanayoandaa ripoti za sera hutumia nguvu katika kuamua mitazamo inayowakilishwa na isiyowakilishwa. Msimamo wao unaweza kuwafanya wapendelee mitazamo na ajenda fulani kuliko zingine.

Matumizi ya lugha yana athari ya moja kwa moja kwa utekelezaji wa programu katika miktadha ya kibinadamu. Kwa mfano, lugha kama vile "kutokana na ushahidi" au "kutokana na data" inaweza kusababisha wakala wa kutekeleza wahisi kama wanahitaji kuthibitisha uhalali wa shughuli za kuzuia na kukabiliana na GBV. Wanaweza kujihisi kama wanashinikizwa kukusanya data za ueneaji wa GBV, hatua ambayo itachukua muda mwingi na yenye gharama kubwa. Pia inaenda kinyume na mwongozo uliopo wa kushughulikia GBV katika miktadha ya kibinadamu, ambao unasema kuwa GBV haihitaji kamwe "kuthibitishwa" ili hatua zichukuliwe.[20] Mfano mwingine ni neno "kuathirika kwa haraka." Katika dharura za kibinadamu, maamuzi kuhusu ni kikundi kipi cha wafadhiliwa au jamii "kinachoweza kuathirika kwa haraka" hufanywa kulingana na vigezo vilivyowekwa na watendaji wa kibinadamu. Kutimiza kipimo hiki cha uwezekano wa kuathirika kwa haraka kuna uhusiano wa moja kwa moja na faida kama msaada wa pesa, lakini dhana hii elekezi ya kuathirika kwa haraka inaficha uchangamano wa yale ambayo watu wanapitia.[21] Neno hilo linaweza pia kutumiwa kama lebo inayoficha miundo na mifumo inayowafanya na kuwadumisha watu katika hali ambapo wanaweza "kuathirika kwa haraka," huku

9 Cornwall & Brock, 1056.

10 Schnable et al., 3.

11 Cronin-Furman, A., et al. "Emissaries of empowerment," Colin Powell School for Civic and Global Leadership, City College of New York, 2-6 (2017); Cornwall & Brock, 1045-1047; Batliwala, S. "Taking the power out of empowerment: an experiential account," *Development in Practice*, 17: 4/5, 557-565 (2007).

12 Cornwall & Brock, 1043.

13 COFEM (2017) 'Reframing language of 'gender-based violence' away from feminist underpinnings', *Feminist Perspectives on Addressing Violence Against Women and Girls Series*, Paper No. 2, Coalition of Feminists for Social Change.

14 Schnable, et al., 4.

15 Ibid, 14-16.

16 Cornwall & Brock, 1052.

17 COFEM "Finding the balance between scientific and social change goals, approaches and methods," Feminist Perspectives on Addressing Violence Against Women and Girls Series, Paper No. 3, (2017) hereafter, COFEM, Finding the Balance.

18 Narayanaswamy, L. "Whose feminism counts? Gender(ed) knowledge and professionalisation in development," *Third World Quarterly*, 37:12, 2158 (2016), hereafter Narayanaswamy; Briggs, J. "The use of indigenous knowledge in Development: problems and challenges," *Progress in Development Studies*, 5:2, 99–114, 107 (2005).

19 Lokot, M. "The space between us: feminist values and humanitarian power dynamics in research with refugees," *Gender & Development*, 27:3, 467-484, 480 (2019), hereafter, Lokot.

20 COFEM, Finding the Balance, 2-4.

21 Johnson, H. "Click to Donate: visual images, constructing victims and imagining the female refugee," *Third World Quarterly*, 32:6, 1015-1037 (2011), hereafter, Johnson.

ikitumiwa kuhalalisha vipaumbele fulani vya ufadhili. Katika muktadha wa kibinadamu, matumizi ya maneno kama “ngono kwa ajili ya manufaa fulani” yanaweza kupunguza ubayana wa safu za mamlaka zinazosababisha dhuluma ya kingono. Vivyo hivyo, kutaja jamii kama “wanufaishwa” hukanusha nguvu na uwezo wa mtu binafsi wa kufanya uamuzi na huwatambulisha watu kama wapokeaji wa misaada wasioweza kujiamulia.

FIKRA ZA KIFEMINISTI

Fikra za kifeministi zinatoa fursa za kuelewa na kushughulikia uhusiano unaotegemeana kati ya mamlaka na lugha katika misaada ya kibinadamu. Ingawa kuna aina kadhaa za ufeministi, wafeministi wanashiriki lengo kuu la kumaliza ukandamizaji wa wanawake na wasichana.[22] Fikra za kifeministi zimejikita katika dhana kwamba safu za mamlaka na udhalimu huchangia uzoefu wa wanawake, wasichana, wanaume, wavulana na watu walio na mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho na namna tofauti ya kujitambulisha kijinsia (SOGIE). Ufeministi una mwelekeo wazi wa kisiasa kwa sababu unalenga kushughulikia mienendo badilifu isiyo sawa ya mamlaka. Hata hivyo, fafanuzi za maendeleo na za kibinadamu zimekosolewa kwa kuondoa ufeministi kutoka kwa maana na dhamira yake ya asili, ili kuufanya ukubalike zaidi.[23]

Ufeministi wakati mwingine huonekana kama dhana ya “Magharibi” ambayo imelazimishwa katika miktadha mingine. Maoni haya yameibua wazo la aina za ufeministi za “mashinani” au za “Kusini”, ambao mara nyingi huonekana kama unatoa njia za kienyeji na za kiasili za kuchora dhana ya ufeministi. Mipango hii, kama vile The African Feminist Charter, imechangia maarifa muhimu ya ufeministi na kusaidia kuangazia utaalamu wa wafeministi kutoka “nchini”.[24] Hata hivyo, wengine wanasema kuwa aina za ufeministi za “Kusini” pia zimeathiriwa na safu za mamlaka na huenda zinawakilisha sauti za “matabaka ya juu” ya wenyeji.[25] Watendaji wa ndani wanaweza kupata faida ya kuwa katika nafasi za mamlaka kwa sababu ya elimu yao, hali yao ya kijamii na kiuchumi, au safu zingine za mamlaka.

Wazo la “ujanibishaji,” ambalo ni muhimu katika uhusiano kati ya uwezo wa kimataifa na wa nchini na ambalo limepata mashiko tangu Mkutano wa Kujadili Masuala ya Kibinadamu Ulimwenguni wa 2016 (World Humanitarian Summit 2016), kwa kutambua mamlaka yanayotumiwa na watendaji wa kibinadamu wa kimataifa (wakiwemo wafadhili na mashirika ya kimataifa yasiyo ya kiserikali (INGOs) juu ya watendaji wa nchini.[26] Licha ya ahadi za ujanibishaji, kwa hali halisi ujanibishaji unaweza kukabiliwa na changamoto kubwa zinazohusiana na mienendo badilifu ya mamlaka, ikiwemo miktadha ya ufurushwaji na ya wakimbizi.[27]

Jinsi mitazamo ya kifeministi inavyochukulia ujanibishaji inaonyesha kuwa kuwepo kwa uhusiano ulio rahisi kubadilika na wenye uaminifu ni muhimu, na kwamba uongozi wa mitaa lazima uwache tu kuchagua wanawake kutoka matabaka ya juu na ujumuishe wanawake kutoka matabaka mengi zaidi. Mitazamo hii inahimiza kwamba lazima kuyapatia mashirika ya nchini mamlaka kuwe na maana na sio tu kufanywa kwa nia ya kufumba macho, na kwamba lazima kuhusishe ushirikiano sawa katika kukubaliana vile “athari” zinazotarajiwa zitakavyokaa.[28] Mijadala hii inasisitiza umuhimu wa kutambua mamlaka katika viwango vingi, sio tu uhusiano kati ya wadau wa kimataifa na wa nchini, lakini pia kati ya watendaji tofauti wa nchini na kati ya watendaji wa nchini na jamii.

Fikra za kifeministi zinaangazia magumu haya yaliyo ndani ya safu za mamlaka, na kutambua kwamba safu za mamlaka na dhuluma zinaweza kutangamana na kuzidisha ukosefu wa usawa katika mamlaka.[29] Kwa mfano, msichana anayebalehe mwenye ulemavu ambaye kwa sasa ni mkimbizi, hupatana na safu za mamlaka zinazohusiana na kuwa mwanamke, kuwa

22 Letherby, G. *Feminist research in theory and practice*. Buckingham: Open University Press, 4 (2003).

23 Cornwall, A. et al. “Gender myths and feminist fables: The struggle for interpretive power in gender and development,” Development and Change, 38:1, 1-20 (2008); Smyth, I. “Talking of gender: words and meanings in development organisations,” *Development in Practice*, 17:4-5, 582-588 (2007).

24 The African Feminist Forum, “The African Feminist Charter,” (2007). Inapatikana mtandaoni: https://awdf.org/the-african-feminist-charter/.

25 Narayanaswamy, 2157.

26 Roepstorff, K. ”A call for critical reflection on the localisation agenda in humanitarian action,” *Third World Quarterly*, 41:2, 284-301 (2020), hereafter, Roepstorff.

27 Pincock, K., Betts, A., & Easton-Calabria, E. ”The rhetoric and reality of localisation: refugee-led organisations in humanitarian governance,” *The Journal of Development Studies*, 13 (2020).

28 Al-Abdeh, M. & Patel, C. “‘Localising’ humanitarian action: reflections on delivering women’s rights-based and feminist services in an ongoing crisis,” *Gender & Development*, 27:2, 237-252, 247-250 (2019).

29 Crenshaw, K. “Mapping the margins: intersectionality, identity politics, and violence against women of color,” *Stanford Law Review*, 43:6, 1241–1299 (1991); Crenshaw, K. “Intersectionality Matters Podcast.” Inapatikana mtandaoni: https://soundcloud.com/intersectionality-matters.

mchanga, kuwa na ulemavu na kuwa mkimbizi — yote kwa wakati mmoja.[30] Neno "utangamano" ni njia ya ufeministi ya kuelewa makutano haya. Utangamano ni zaidi ya kutambua tu tofauti kati ya vikundi fulani, kama inavyofanyika wakati mwingine katika mazingira ya kibinadamu. Badala yake, umejikita wazi katika kuelewa na kubadilisha ukosefu wa usawa katika mamlaka.[31]

Fikra za kifeministi zinatambua kuwa safu za mamlaka zinaathiri yale yanayojulikana kuhusu jamii. Wafeministi wanasema kuwa katika historia, maarifa yameendelezwa kwa "mtazamo wa wanaume," na kuathiri jinsi ulimwengu unavyoeleweka.[32] Katika misaada ya kibinadamu, jambo hili lilimaanisha kuwa michakato ya kuelewa mahitaji ya jamii wakati mwingine imezipatia nafasi sauti za wanaume, ambao mara nyingi ndio viongozi wa jamii, viongozi wa dini, au walinda lango, badala ya wanawake na wasichana. Jambo hili wakati mwingine limetokea chini ya dai la kuheshimu utamaduni wa wenyeji. Wafeministi wanahimiza kwamba mahitaji na mitazamo ya wanawake na wasichana ni mahusus na yanathaminiwa, badala ya kulazimishwa na wale walio katika nafasi za mamlaka. Hii inamaanisha kuwa kufanya uchambuzi wa kijinsia unaoangazia vigezo vinavyotangamana, badala ya kuchukulia tu dhana fulani juu ya watu au jamii, ni desturi muhimu ya kifeministi. Ingawa kujifunza kutoka kwa miktadha mingine kunasaidia, ni muhimu kwamba programu zijumuishe hali halisi ambazo wanawake na wasichana na jamii zenyewe zimepitia.

Sio tu matokeo au maafikiano ya mwisho yanayowapatia wasiwasi wafeministi, lakini pia michakato inayohusika katika kufikia matokeo.[33] Hivyo basi, wafeministi wanapinga njia zinazokubalika za kukusanya, kufuatilia na kutathmini data, au kufanya utafiti katika mazingira ya kibinadamu. Wafeministi, ambao wanakosoa kutia msisitizo katika kupata "ushahidi" kwa kushirikisha jamii wakati mwingine kwa njia zisizo za moja kwa moja, wanalenga njia za kimahusiano ambazo zinapea kipaumbele uhusiano badala ya mahitaji kama "thamani ya pesa."[34] Huenda mawazo ya kifeministi yakavuruga njia za kawaida za kuelewa masuala — kwa mfano, matumizi ya tathmini za haraka katika mazingira ya kibinadamu. Badala yake, wafeministi wanapendekeza kuwa ni muhimu kuchukua muda kuruhusu maswala yanayokabili jamii yajitokeze, wakati ambao jamii zitajihisi ziko tayari kushiriki habari kama hizo, ikiwa zitahisi hivyo.[35] Mbinu hii inahitaji kutumia njia ambazo ni rahisi kubadilika, zinazowezesha ushiriki wenye maana.[36] Wafeministi wanasisitiza kuwa ushirikiana na jamii unapaswa kujikita katika kutendeana - kutoa na kupokea - kama njia ya kusawazisha mienendo badilifu ya mamlaka kati ya wale wanaokusanya data na wale wanaotoa data.[37]

Fikra za kifeministi zimetoa mtazamo huu kwenye mazoezi ya kujitathmini. Kujitathmini kunajumuisha kujilenga ndani kwa kutafakari kwa kina jinsi nafasi, asili na uzoefu wetu unavyoweza kuathiri mitazamo, mielekeo na upendeleo wetu. Ndani ya misaada ya kibinadamu, inamaanisha pia kutambua jinsi utoaji nafasi katika taasisi unaweza kuathiri mamlaka (au ukosefu wa mamlaka). Kujitathmini kunamaanisha kutambua safu changamano za mamlaka ambazo zinaathiri utoaji misaada ya kibinadamu, ikiwemo jinsi vipaumbele vya wafadhili vinavyoathiri uandaaji wa programu. Baadhi ya wataalamu wanapendekeza kuwa mawazo ya kifeministi yameathiriwa na ajenda za masoko huru katika miktadha ya maendeleo na masuala ya kibinadamu, na kusababisha kutilia mkazo kwa wanawake na wasichana kama wazalishaji wa utajiri wa kiuchumi.[38] Kutafakari juu ya jukumu la wafadhili na wengine walio na ushawishi juu ya rasilimali za misaada kunamaanisha kutambua safu hizi za mamlaka na kuzipinga, panapowezekana.

UFUPISHO

30 Mpango wa Building Local Thinking Global (BLTG), "Kujitayarisha na Kushughulikia Visa vya Unyanyasaji wa Kijinsia katika Miktadha ya Dharura. Mwongozo wa ujumuishaji wa wanawake na wasichana anuai," (2019). Inapatikana mtandaoni: http://gbvresponders.org/wp-content/uploads/2020/01/Inclusion-Guidance-Note-_Swahili.pdf.

31 COFEM, "COFEM Feminist Pocketbook Tip Sheet #1. Why does a feminist perspective matter in work to prevent and respond to violence against women and girls?," (2018) Available online: https://cofemsocialchange.org/wp-content/uploads/2018/11/TS1-Why-does-a-feminist-perspective-matter.pdf; Michelis, I. "'Picked up, misused, abused, changed': intersectionality in the humanitarian discourse on gender-based violence," (2020).

32 Brooks, A. "Building knowledge and empowerment through women's lived experience," in Leavy, P. L. and Hesse-Biber, S. (eds) *Feminist research practice: a primer*. London: SAGE Publications Ltd, 53–82, 68 (2006).

33 Interpares, Action Canada, & Oxfam Canada "A feminist approach to Canada's international assistance," (2016). Inapatikana mtandaoni: https://www.awid.org/sites/default/files/atoms/files/statement-a_feminist_approach.pdf.

34 Lokot, 477-480.

35 Trinh, Minh-ha, Woman, Native, Other: *Writing Postcoloniality and Feminism*, Bloomington and Indianapolis: Indiana University Press, 1 (1989).

36 Liamputtong, P. *Researching the vulnerable. A guide to sensitive research methods*. London: SAGE Publications Ltd, 13 (2007).

37 Huisman, K. "'Does this mean you're not going to come visit me anymore?': an inquiry into an ethics of reciprocity and positionality in feminist ethnographic research," *Sociological Inquiry*, 78:3, 372–396 (2008).

38 Calkin, S. "Feminism, interrupted? Gender and development in the era of 'smart economics,'" *Progress in Development Studies*, 15:4, 295-307, 297 (2015).

MATOKEO

MANENO YA KAWAIDA NA SAFU ZAKE ZA MAMLAKA

Katika utafiti huu, wahojiwa waliulizwa wajibu kuhusu jinsi wanavyohisi wanaposikia maneno fulani katika sekta ya kibinadamu, ambayo hutumiwa kuelezea watu binafsi, vikundi au mashirika. Waliulizwa wakague orodha ya maneno na wajibu kulingana na kiwango cha: wasiwasi sana, wasiwasi kiasi, bila maoni yoyote, bila wasiwasi au bila wasiwasi hata kidogo. Maneno matano ya juu ambayo washiriki wengi walikuwa na wasiwasi sana nayo ni: “mwathiriwa,” “za kipato cha chini,” “waliotengwa,” “wachache,” na “kuathirika kwa haraka.” Sehemu zifuatazo zinachambua maneno haya kwa undani zaidi, pamoja na maneno mengine ya kawaida yaliyojadiliwa na washiriki katika mahojiano, majadiliano ya vikundi na utafiti.

MNUFAISHWA

Katika utafiti huu, asilimia 23 ya wahojiwa walisema kuwa wana wasiwasi kiasi au mwingi kuhusu neno "mnufaishwa." Karibu asilimia 29 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 49 hawakuwa na wasiwasi wowote.

Katika vikundi vyote vitatu vya majadiliano, kulikuwa pia na hisia tofauti juu ya neno “mnufaishwa.” Wengi waliona kuwa si nzuri wala mbaya. Washiriki wachache katika majadiliano ya vikundi waliona neno hilo lilikuwa nzuri: “Kitu kizuri kinachomfaidi mtu” (Afrika Mashariki). Mshiriki mmoja katika majadiliano ya vikundi alisema, “Wanufaishwa linamaanisha kuwa mtu anapata faida kutoka kwa mipango au vitendo fulani” (Asia). Mshiriki mwingine katika majadiliano ya vikundi alitoa maoni kwamba neno hilo lilikuwa “bora kuliko ‘mfadhiliwa (donee)’—mtu anayepokea ufadhili au anayepokea msaada” (Asia).

Kwa upande mwingine, washiriki wengine wa majadiliano ya vikundi walizungumza juu ya maana hasi ya neno hili: “Ni kama tunawapatia msaada” (Afrika Mashariki). Mshiriki mwingine wa majadiliano ya vikundi alipendekeza kuwa neno hilo linaweza kuwa la kisiasa: “Ni kama sisi hatutambui kwamba wanaonufaishwa au jamii ni washirika sawa na sisi na pia wana rasilimali, na tunaweza kushirikiana ili kufikia lengo husika” (Asia). Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi aligusia tafsiri ya neno kutoka Kiingereza: “Tunapolitafsiri kwa lugha yetu halina maana kwa sababu linatumika kuwarejelea wanaonufaishwa na bima” (Asia). Mshiriki mmoja wa mahojiano pia alisema kuwa neno hili lina “mwelekeo wa uhisani” (Afrika Mashariki). Mhojiwa mmoja wa utafiti alisema, “Mnufaishwa pia linamaanisha kutegemea huduma za wengine” (Asia).

Mshiriki mwingine wa majadiliano ya vikundi ambaye alihisi neno hilo haliegemei upande wowote alipendekeza kwamba muktadha ambapo “mnufaishwa” linatumiwa huamua ikiwa linafaa, akielezea kuwa ni sawa kutumia neno hilo katika sekta ya kibinadamu, lakini sio katika kazi ya utetezi, ambapo neno ambalo lingependelewa ni “mshiriki katika shughuli” au “mdau” (Afrika Mashariki). Mshiriki mwingine wa majadiliano ya vikundi alipendekeza neno “mshirika” (Asia). Washiriki wachache wa majadiliano ya vikundi walipendekeza “walengwa” au “kundi lengwa” kama maneno mbadala, lakini mshiriki mwingine aliona, “Labda

kufikiria wanawake au watoto kama walengwa linaweza kuwa tatizo” (Mashariki ya Kati). Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema kwamba “kulenga” wanawake na wasichana inasikika “kana kwamba ni vitu vya kupigwa risasi” (Afrika Mashariki). Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alipendekeza “wenye haki” na “wanaobeba majukumu” kama vibadala kwa sababu yanathibitisha wazo kwamba watu wana haki huku watendaji tofauti katika sekta ya kibinadamu wana majukumu wanayofaa kuwatimizia (Mashariki ya Kati).

Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alisema: “Nadhani neno hili limetumika sana na limekuwa la kawaida katika [sekta] ya kibinadamu kiasi kwamba maana yake haiegemei upande wowote. Hatujiulizi, linamaanisha nini? ” (Mashariki ya Kati). Mshiriki mwingine wa majadiliano ya vikundi aliongezea, “Labda kwa sababu tunaamini kile tunachofanya, hivyo hatuzingatii kwa undani maana ya neno” (Mashariki ya Kati).

KUJENGA UWEZO

Katika utafiti huu, asilimia 11 ya waliohojiwa walisema wana wasiwasi na neno "kujenga uwezo". Karibu asilimia 17 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 71 hawakuwa na wasiwasi wowote.

Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema kujenga uwezo kunamaanisha “kuhamisha watu kutoka hatua moja hadi nyingine.” Aliongeza, “Linakaribiana na uwezeshaji” (Afrika Mashariki).

Mshiriki mmoja wa mahojiano alijadili jinsi wanajiepusha na neno “kujenga uwezo” wakati wa kualika wadau kama polisi. Walakini, hutumia neno hilo wakati wanazungumza na jamii, jambo ambalo alihisi lilikuwa tatizo: “Wakati wa kufanya kazi na vikundi vilivyotengwa, ni rahisi kusema kujenga uwezo, tunahitaji kuwa na mafunzo. Akilini mwetu ni kama wanahitaji kujenga uwezo na ni sawa kuwaambia. Lakini tunapowasiliana na polisi, tunahitaji kuliondoa” (Mashariki ya Kati).

Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema hakukuwa na mtazamo wowote hasi uliohusishwa na neno kujenga uwezo (Asia). Mwingine alibaini pande chanya na hasi: “Ikiwa unataka kuangalia maana kwa undani zaidi au kuliangalia katika muktadha wa mamlaka, basi kujenga uwezo kunakuwa wewe ndiwe mwenye uwezo na utawasaidia wengine kuimarisha uwezo wao kwa sababu uliwakuta bila chochote… jambo ambalo si la kweli, watu wana uwezo wao” (Afrika Mashariki). Mhojiwa wa utafiti alisema kuwa “kujenga uwezo kunamaanisha hakuna uwezo uliopo” na akapendekeza “kukuza uwezo” kama neno mbadala (Asia). Mhojiwa mwingine wa utafiti alipendekeza neno “kuimarisha uwezo” (Asia).

Mshiriki mwingine wa mahojiano alisisitiza kuwa kwake, ujenzi wa uwezo ulihusisha “pande zote mbili” na “sio upande mmoja pekee” (Afrika Mashariki). Alisema kuwa kujenga uwezo ni “jambo moja katika istilahi za maendeleo ambalo kila mtu anategemea” lakini akasisitiza kuwa “bila huduma saidizi, kujenga uwezo peke yake hakuwezi kubadilisha au kuwa na athari kubwa katika kazi ya maendeleo.” Wakati wa kujadili juu ya ufeministi, alirejelea dhana ya kujenga uwezo: “Katika mazungumzo au mchakato wowote tunaohusika, tunahitaji kuhakikisha tunavunja safu zilizopo, tunachambua upya safu hizo. Ikiwa wewe ni mkufunzi, unafanya semina ya kujenga uwezo, haimaanishi kuwa taarifa ulizo nazo ni za kuaminika kuliko zile za watu unaowafundisha” (Afrika Mashariki).

UWEZESHAJI

Katika utafiti huu, asilimia 3 ya wahojiwa walisema kuwa wana wasiwasi na neno "uwezeshaji." Karibu asilimia 14 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 83 hawakuwa na wasiwasi wowote.

Washiriki wengi walitaja kwamba “uwezeshaji” ni neno zuri. Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema kwamba, “Sanasana linahusu uwezo wa kuchukua hatua na maamuzi ambayo yanaathiri maisha yako mwenyewe. Ni mchakato. Pia huathiri jinsi unavyohisi” (Afrika Mashariki). Mshiriki mwingine wa mahojiano alifafanua, “Maadamu halitumiwi kama daraja kutoka kwa udhaifu kwenda kwa nguvu,” akidokeza kuwa wakati mwingine kuna “kidokezo hasi kwamba mtu ni dhaifu” na anahitaji uwezo wake uimarishwe (Mashariki ya Kati). Wengine walitumia maneno ‘kujenga uwezo’ na ‘uwezeshaji’ kwa kubadilishana: “Matokeo ya kumwezesha mtu, au kujenga uwezo, naona ni mazuri. Tunajenga uwezo wao wa kutetea haki zao. Tunawapa maarifa ambayo wanaweza kutumia kupata haki zao. Kuna uwezekano kwamba wale wanaowezeshwa wanaweza kuwawezesha wengine pia” (Asia).

Washiriki wachache waliona kuwa neno uwezeshaji linaweza kutumiwa vibaya kuficha shughuli za mafunzo, lakini huenda mafunzo yasiwe ya kutosha kuhakikisha uwezeshaji. Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema kuwa neno hilo "wakati mwingine hutiliwa chumvi au kuthaminiwa zaidi ya inavyostahili": "Uwezeshaji ndio mtindo mpya baada ya kujenga uwezo au kuimarisha ujuzi, lakini je, hatua zinazotolewa zinawezesha watu kweli?" (Mashariki ya Kati). Mshiriki mwingine wa mahojiano alisema: "Daima tunatumia na kusikia neno hili. Haimaanishi kuwa kumwezesha mtu ni kumpa semina ya ufahamu. Maana yake si hii kila wakati. Ikiwa tunazungumza juu ya uwezeshaji, lazima tuzungumze juu ya mpango wala si mradi... Uwezeshaji hautakuwa iwapo nitafanya semina hii mwaka mmoja halafu mwaka ujao kuwe hakuna ufadhili" (Mashariki ya Kati). Mshiriki mwingine wa mahojiano alisema kuwa uwezeshaji unapotekelezwa vyema, unaweza kushughulikia visababishi vikuu vya shida (Afrika Mashariki).

Mshiriki mmoja wa mahojiano alizungumza kuhusu shinikizo kutoka kwa wafadhili kutumia neno hili: "Wakati mwingine tunalazimika kulitumia. Wakati tunatuma miswada, lazima tulitumie ikiwa mada kuu ni uwezeshaji au lengo ni uwezeshaji… Tuliamua kutotumia neno 'uwezeshaji' miaka miwili iliyopita. Tunaamini kila mtu ana uwezo, ana nguvu ndani yake, anaweza, lakini tunapaswa kuwaruhusu waelewe na wagundue nguvu hii waliyo nayo. Tunawaimarisha ili wajielewe wenyewe, watumie rasilimali walizo nazo." (Mashariki ya Kati). Mshiriki mwingine wa mahojiano pia alitaja kwamba shirika lao lilikuwa limeacha kuangazia uwezeshaji wa wanawake kiuchumi na kuegemea upande wa haki ya kiuchumi ili kutambua jinsi mamlaka yanavyochangia katika maisha ya wanawake (Afrika Mashariki).

KUTOKANA NA USHAHIDI

Katika utafiti huu, asilimia 6 ya waliohojiwa walisema kuwa wana wasiwasi kiasi au mwingi kuhusu neno "kutokana na ushahidi." Karibu asilimia 26 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 69 hawakuwa na wasiwasi wowote.

Neno 'kutokana na ushahidi' pia lilijadiliwa wakati wa majadiliano ya vikundi. Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi aliona migawanyiko ya kisiasa ya kutumia neno hili: "Linaweza kuwa suala nyeti kidogo kwa serikali ikiwa tutatumia 'kutokana na ushahidi' au 'kwa misingi ya ushahidi' kwa sababu hatuna maneno haya katika nchi yetu. Serikali inaweza kuhisi kuwa kuna mtu anayetaka kuwachunguza au kupata ushahidi wa kuingilia kati katika sera au siasa" (Asia).

Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema "kutokana na ushahidi" lilikuwa neno bora kuliko "kutokana na data," akielezea jinsi wazo la data linaweza kusababisha maoni ya wanawake kutengwa (Afrika Mashariki). Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alibaini: "Data inaweza kusomwa kwa njia tofauti. Inaweza pia kusomwa vibaya au kusoma zaidi. Kwa hivyo, kutegemea sana vitu hivi pia kunaweza kusababisha kupuuza kabisa sehemu zingine ambazo pia ni muhimu na ambazo hazionyeshwi katika data" (Mashariki ya Kati). Pia alisema kuwa ni muhimu kutowasilisha tu takwimu kwa wafadhili lakini kuandaa mikutano maalum ya "kuchambua kwa kina" na kujadili tofauti ndogo zilizoko.

UJANIBISHAJI

Katika utafiti huu, asilimia 17 ya waliohojiwa walisema kuwa wana wasiwasi kiasi au mwingi kuhusu neno "ujanibishaji." Karibu asilimia 29 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 54 hawakuwa na wasiwasi wowote.

Washiriki kadhaa wa mahojiano na majadiliano ya vikundi walijadili dhana ya ujanibishaji. Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema, "Ujanibishaji haufaulu hapa kwa sababu hakuna mtu anayeuunga mkono. Wafadhili hawaamini Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya hapa nchini, na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Kimataifa hayataki kutugawia sehemu ya fedha zao" (Asia). Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema kuwa wafadhili wako tayari kupatia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Kimataifa pesa nyingi kuliko Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya nchini (Afrika Mashariki). Mshiriki mwingine wa mahojiano alizungumzia changamoto zinazoyakabili mashirika madogo madogo ya nchini: "Mashirika mengi Yasiyo ya Kiserikali ambayo ni makubwa ndani mwa nchi, na ambayo yanaweza kufikia nafasi za kujenga uwezo huwa kila mara yanashinda miswada hii kwa sababu yanajua namna ya kuandika na namna ya kutekeleza. Mashirika mengine madogo hayapati fursa za kupata ufadhili huu" (Asia). Ni mtu mmoja tu aliyekuwa na

maoni mazuri juu ya wafadhili: “Hapo awali, njia ya wafadhili ilikuwa tofauti kabisa, walikuwa na vikwazo vingi zaidi. Sasa wanatuchukua kama washirika. Sasa wanasema, “Tunashirikiana.” Jambo hili liliziba pengo kati ya wafadhili na mashirika yanayofanya utekelezaji” (Asia).

KUTENGWA

Katika utafiti huu, asilimia 66 ya wahojiwa walisema kuwa wana wasiwasi kiasi au mwingi kuhusu neno "kutengwa. Karibu asilimia 9 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 26 hawakuwa na wasiwasi wowote.

Mshiriki mmoja wa mahojiano alielezea sababu za neno hili kutumiwa: “Tunalitumia kwa watu ambao wako katika hali duni na wanyonge” (Asia). Wengine walijadili maana hasi ya neno hilo. Mshiriki mmoja wa mahojiano alipendekeza kuwa kuelezea watu kama waliotengwa kunapitisha aina fulani ya hukumu kwa jamii na kupendekeza kuwarejelea kama waliokosa nafasi ya kufikia rasilimali au ambao hawajafikiwa au wasio na bahati: “Si tatizo lao kuwa wako mbali na hawana nafasi ya kufikia huduma. Ni tatizo letu kwa sababu hatukuwafikia hapo awali, au serikali haikuwafikia. Tunaposema kutengwa, ni kama kosa ni lao” (Mashariki ya Kati). Mshiriki mwingine wa mahojiano alisema: “Neno hili linadokeza kutokuwa na nafasi muhimu katika jamii. Ni aina ya ubaguzi…. Katika Mkutano wa Kibinadamu Ulimwenguni, tulianza kutumia ‘watu walioathirika’” (Asia).

Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alisema kuwa vijana na wanawake wakati mwingine huelezewa kama waliotengwa, lakini “kwa kweli hawajatengwa.” Alielezea ni kwa nini neno hili linatumika visivyo: “Tunachonuia kusema ni kuwa hawana fursa sawa, lakini tunatumia neno kutengwa... Neno hili linadokezea udhaifu lakini kwa kweli, wao si dhaifu. Wana nafasi chache lakini wana uwezekano sawa, uwezo sawa na wakati mwingine zaidi. Kwa hivyo, neno hili halina maana halisi ya kile tunachotaka kusema” (Asia).

Washiriki wengi walisisitiza kwamba neno “kutengwa” linahitaji muktadha: “Natamani kungekuwa na neno lingine kando na kutengwa. Kulingana na muktadha ambamo linatumiwa… Unaposema kutengwa unaweza kuwa unaelezea kuwa vikundi fulani havijajumuishwa. Kutengwa kunategemea sana muktadha. Linaweza kumaanisha kuwa shughuli zingine hazijumuishi wote” (Afrika Mashariki); na “Ni vizuri kuangalia ni kwa nini wametengwa, wanakabiliwa na changamoto zipi” (Mashariki ya Kati).

Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alitafakari juu ya kazi yake inayohusisha jamii za wakimbizi, hasa ukweli kwamba hata wale walio katika maeneo ya mbali hawatajiita waliotengwa. Alidadisi wazo kwamba kuishi maeneo ya mijini kunamaanisha “kuishi katika kituo kikuu”: “Maneno yote tunayotumia kuyaelezea yanahusiana nasi. Tunakaa [jina la jiji] na tunafikiria ndio kituo kikuu. Wafadhili wetu ambao wanakaa kule [jina lingine la jiji] wanafikiri ndio kituo kikuu. Wafadhili wetu wa kimataifa kule [jina la jiji la Uropa] wanafikiri ndio kituo kikuu. Inafurahisha sana kuona kwamba mamlaka hubadilika na kituo kikuu hubadilika pia” (Mashariki ya Kati). Mshiriki mwingine wa mahojiano alisema, “Mtu anayetumia neno anaonekana kuwa na nguvu zaidi kuliko yule anayepokea neno” (Afrika Mashariki).

WACHACHE

Katika utafiti huu, asilimia 51 ya wahojiwa walisema kuwa wana wasiwasi kiasi au mwingi kuhusu neno "wachache." Karibu asilimia 31 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 17 hawakuwa na wasiwasi wowote.

Washiriki wachache walitaja changamoto zinazotokana na kutumia neno “wachache.” Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alisema neno hilo lilitumiwa sana lakini lilileta shida katika maingiliano na jamii: “Wao husema, ‘Msituite wachache, sisi sio wachache, sisi ni raia sawa. Kwa kutuita wachache mnatufanya kuwa wadogo… ‘ Baada ya haya, nilianza kutumia ‘mtu wa dini nyingine’ kwa sababu nilihisi kuwa neno hili haliwafanyi wajihisi vizuri” (Asia). Katika mfano huu, kusikia moja kwa moja kutoka kwa jamii kulimfanya abadilishe lugha aliyokuwa akitumia.

Mshiriki wa mahojiano alisema: “Kubadilisha kikundi chenye uwezo na kukifanya kuwa kategoria moja ya wachache kunavua watu haki zao. Wakati mwingine hufanywa kwa nia nzuri lakini bado huweka watu kwenye vitengo fulani ambavyo huzuia uwezo wao” (Mashariki ya Kati).

KUSHIRIKI

Katika utafiti huu, asilimia 3 ya wahojiwa walisema kuwa wana wasiwasi kuhusu neno "kushiriki." Karibu asilimia 3 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 94 hawakuwa na wasiwasi wowote.

Wakati wa kikao cha uthibitishaji, washiriki walijadili dhana ya kushiriki. Mshiriki mmoja alisema, "Kushiriki, kwangu kunamaanisha mimi ni sehemu ya kitu fulani, nina nafasi katika jambo hili" (Afrika Mashariki). Mwingine alizungumzia juu ya "kushughulika kwa kutenda" kama njia ya kufafanua kushiriki (Afrika Mashariki). Maoni haya yalikuwa sawa na ya mshiriki wa mahojiano ambaye alihisi neno "kushughulika" linahusisha "uchukuaji hatua zaidi" kuliko kushiriki (Asia).

Washiriki katika kikao cha uthibitishaji pia walijadili jinsi neno "kushiriki" linavyoweza kutumiwa vibaya. Mshiriki mmoja aliakisi: "Linaweza kutumiwa vibaya iwapo litarejelea tu kuhusika. Kuhusika kunaweza kumaanisha nilikuwepo, nilishiriki… Lakini basi kushiriki kunaweza kosa maana wakati neno hili linarejelea tu kuwakilisha wala sio kushughulika kwa kutenda, hakuna kushiriki katika kufanya uamuzi... Kushiriki tu na kuwakilishwa bila sauti halisi kunaweza pia kukosa maana" (Afrika Mashariki). Mshiriki mwingine alisema kuwa neno 'kushiriki' linaweza kutumiwa vibaya "wanapokuuliza ushiriki lakini wanapuuza utaalamu na maoni yako." Alielezea: "Jambo hili huwa linatokea mara nyingi… Mashirika ya haki za wanawake yanaombwa kushiriki… Halafu shirika linahusika, linashiriki utaalamu, maoni, linatoa uchambuzi wa kina wa hali katika muktadha halisi... Lakini ujuzi huu unapohamishwa, huwa kwa njia fulani unatapanyika, huwa unapotea na haufikii viwango vya maamuzi." Katika kutafakari juu ya maadili ya ufeministi, alipendekeza kuzingatia kupata njia za kushirikiana kupitia mbinu za ushirikiano kutoka chini kuelekea juu ili kila mtu ahisi anajumuishwa na "ana nafasi ya kuchangia maoni yake katika jambo hili, amechangia." Alisema, "Suala hili linahusu zaidi kujenga uhusiano kuliko tu kuangalia matokeo mazuri ya mradi" (Mashariki ya Kati). Mshiriki mmoja alipendekeza kwamba neno "ubia" linapaswa kutumiwa na wafeministi mara nyingi kuliko neno "kushiriki."

MKIMBIZI

Katika utafiti huu, asilimia 46 ya wahojiwa walisema kuwa wana wasiwasi kiasi au mwingi kuhusu neno "mkimbizi." Karibu asilimia 29 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 26 hawakuwa na wasiwasi wowote.

Wakati wa kikao cha uthibitishaji, washiriki walijadili neno "mkimbizi." Mshiriki mmoja alitaja kwamba neno hilo linahusishwa na ufurushwaji (Asia). Mshiriki mwingine alitaja kwamba chanzo cha neno hilo ni Umoja wa Mataifa (Afrika Mashariki). Washiriki wachache kutoka eneo la Mashariki ya Kati waliona kuwa neno "mkimbizi" linahitaji kudumishwa ili kunasa maana ya kisiasa ya neno hilo, ambayo ni muhimu sana kwa Wapalestina ambao wamelazimika kuhama makwao.

Washiriki wachache pia walitaja unyanyapaa unaohusishwa na neno hilo. Mshiriki mmoja alisema: "Jina mkimbizi, kwetu linamaanisha kwamba sisi si wa hapa. Sisi si raia wa nchi na unachukuliwa kama 'mwingine,' kama wewe si mwanadamu… Unajisikia kama wewe sio wa huko, na hauna haki ya kupata vitu kama raia wa nchi hiyo" (Afrika Mashariki). Mshiriki mwingine alisema kwamba neno hili linaathiri jamii kwa njia mahususi: "Baada ya kurejeshewa maisha ya kawaida, wanaendelea kufikiria wao ni wakimbizi… Bado wanasubiri mashirika yawasaidie kwa sababu wao ni wakimbizi au ni wahamiaji. Daima huwafanya wajione dhaifu na kwamba kuna mtu mwingine aliye na rasilimali ya kuwapatia" (Afrika Mashariki).

Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alisema neno mbadala wanalotumia ni "watu wa kuzingatiwa" (Afrika Mashariki).

USTAHIMILIVU

Katika utafiti huu, asilimia 3 ya wahojiwa walisema kuwa wana wasiwasi mwingi kuhusu neno "ustahimilivu." Karibu asilimia 20 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 77 hawakuwa na wasiwasi wowote.

Neno ustahimilivu lilijadiliwa kidogo katika mahojiano na majadiliano ya vikundi. Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema: "Ni neno zuri kwa sababu linapatia nguvu. Halizungumzii udhaifu" (Mashariki ya Kati). Mshiriki mwingine wa mahojiano aliangazia changamoto zinazohusiana na neno hili: "Ni kama unasema, jikaze kamba na utafute namna ya kuvumilia. Kisaikolojia lina maana, lakini vinginevyo katika kazi yetu ya uwezeshaji huenda likahitaji kufafanuliwa zaidi" (Afrika Mashariki). Mshiriki mwingine wa mahojiano alisema: "Kwa nini jamii zinapaswa kuendelea kustahimili shida? Kwa nini hatufanyi kazi kuhakikisha kuwa tunawaondoa watu kutoka kwenye umaskini badala ya kuimarisha uwezo wao wa kustahimili shida na kujiinua tena?" (Afrika Mashariki).

ZA KIPATO CHA CHINI

Katika utafiti huu, asilimia 69 ya waliohojiwa walisema kuwa wana wasiwasi kiasi au mwingi kuhusu neno "ya kipato cha chini." Karibu asilimia 20 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 11 hawakuwa na wasiwasi wowote.

Mhojiwa mmoja wa utafiti alielezea, "Kuhusu ni nani mwenye kipato cha chini, na kwa nini na ni nani anayedhania kwamba Ulaya au Amerika ni mifano ya ustaarabu, maisha bora ambayo kila mtu anatamani" (Mashariki ya Kati). Mhojiwa mwingine wa utafiti alisema neno hili "linaonyesha uhusiano na ukuu wa kimamlaka" (Asia). Mhojiwa mwingine wa utafiti alipendekeza, "Ingefaa kutaja kila nchi kwa jina lake… Afrika Kaskazini, Uarabuni, ulimwengu wa Kiislamu, Amerika ya Kusini… bila kutaja kipato cha juu au cha chini" (Mashariki ya Kati). Mhojiwa mmoja wa utafiti alipendekeza Kaskazini-Kusini kama kibadala (Mashariki ya Kati), ingawa wengine walitaja wasiwasi wao kuhusiana na neno hili. Mhojiwa mwingine wa utafiti alipendekeza "nchi zenye uchumi unaokua" (Mashariki ya Kati).

JADI

Katika utafiti huu, asilimia 23 ya waliohojiwa walisema kuwa wana wasiwasi kiasi au mwingi kuhusu neno "jadi." Karibu asilimia 40 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 37 hawakuwa na wasiwasi wowote.

Washiriki wa majadiliano ya vikundi walijadili jinsi neno "jadi" linavyoweza kuwa chanya au hasi. Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alizungumzia jinsi linavyoweza kurejelea vitu vizuri, kama historia, mavazi au vyakula (Mashariki ya Kati). Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alipendekeza kwamba neno hilo lilihusishwa na "kitu kilichopitwa na wakati, kitu ambacho hakijapigwa msasa, kitu ambacho sio cha kisasa hata kidogo" (Afrika Mashariki).

Mshiriki mwingine wa majadiliano ya vikundi alidokeza kwamba neno hili "hufanya watu waonekane kana kwamba ni wahafidhina" (Afrika Mashariki). Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alidokeza kwamba huenda neno hilo lisionekane chanya kwa jamii: "Ikiwa tutataja desturi hasi za jadi, huenda ikawa na madhara kwa baadhi ya jamii… Ukitafsiri kwa lugha ya wenyeji, huenda watu wakadhani kuwa hawajafikiwa na maendeleo" (Asia). Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alisema kuwa kutumia neno "jadi" kuelezea kikundi kunaweza "kukitenga" wakati kuna makabila mengi tofauti katika kikundi hicho, na kupendekeza badala yake kutumia rasilimali za eneo husika, jamii ya eneo husika au wadau wa eneo husika (Afrika Mashariki).

Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alisema, "Wakati mwingi hasa katika sekta ya kibinadamu sijaona neno jadi likitumika kwa njia chanya" (Afrika Mashariki). Alielezea kuwa neno hilo hutumiwa mara nyingi kumaanisha "kitu ambacho watu wanapaswa kuachana nacho," akidokeza kuwa hili ni neno ambalo si "thabiti" na ambalo watu hutumia bila kufikiria muktadha.

Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alisisitiza haja ya kufafanua neno hili ili kuhakikisha maana inayofaa inawasilishwa (Afrika Mashariki), huku mwingine akipendekeza kwamba muktadha ni muhimu na lazima kuwe na "ufafanuzi ili lisidhuru au kutoa maoni potofu" (Afrika Mashariki).

MWATHIRIWA

Katika utafiti huu, asilimia 71 ya wahojiwa walisema kuwa wana wasiwasi kiasi au mwingi kuhusu neno "mwathiriwa." Karibu asilimia 17 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 11 hawakuwa na wasiwasi wowote.

Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema: “Manusura ni bora. Inamaanisha kuwa ana matumaini, ana nguvu za kubadilisha hali yake” (Mashariki ya Kati). Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alielezea kuwa waathiriwa “hutambuliwa kulingana na madhara yaliyowapata,” huku manusura “hutambuliwa kulingana na maisha yao baadaye” (Mashariki ya Kati). Alipendekeza kuwa neno manusura linaonyesha nguvu katika kuishi baada ya tukio la vurugu. Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alitaja neno “mteja” kama kibadala cha “mwathiriwa” (Asia).

Mshiriki mwingine wa mahojiano aliangazia tafsiri ya neno hili: “Kwa Kiingereza, tunatumia neno, ‘manusura,’ kurejelea wanawake ambao wamepitia vurugu. Wakati wanatafsiri neno hili kwa Kiarabu, linamaanisha wanawake ambao walitoroka vurugu, lakini kwa kweli bado wanapitia vurugu. Hawakuweza kuitoroka. Kusema mwathiriwa, ni kama mwanamke huyo ni dhaifu sana. Lakini tunapotumia manusura kwa Kiarabu, haliibui maana sawa kwa Kiingereza” (Mashariki ya Kati).

KUATHIRIKA KWA HARAKA

Katika utafiti huu, asilimia 71 ya wahojiwa walisema kuwa wana wasiwasi kiasi au mwingi na neno "kuathirika kwa haraka." Karibu asilimia 17 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 11 hawakuwa na wasiwasi wowote.

Mshiriki mmoja wa mahojiano alielezea ni kwa nini neno hili linatumiwa: “Tunapozungumza juu ya wakimbizi, kwa kuwa walihama kutoka eneo moja kwenda lingine, wanaweza kuathirika kwa haraka kwa sababu wao si raia. Hawana hadhi katika eneo husika.” Alielezea kuwa maneno kama ‘kuathirika kwa haraka’ yanaweza kuashiria kwamba vikundi vingine “vinastahili zaidi” (Asia).

Washiriki wachache wa mahojiano walisema kuwa neno ‘kuathirika kwa haraka’ linahusishwa na udhaifu (Asia). Mhojiwa wa utafiti pia alisema kuwa hili ni neno “lisiloibua taswira ya kina” ambalo halisemi chochote zaidi juu ya sababu za kuathirika kwa haraka (Mashariki ya Kati). Mshiriki mmoja wa mahojiano alijadili jinsi kutumia neno hili kunaweza kuwa tendo la nguvu kwa kundi lingine: “Kuwa nje ya vikundi hivi, wakati wewe hauko katika hatari ya kuathirika kwa haraka... ni rahisi kuwaweka wengine wote chini ya kitengo hiki. Hapa ndipo safu ya mamlaka inadhihirika… Hata ikiwa jambo hili limefanywa kwa nia njema, bado unajitenga na vikundi hivi” (Mashariki ya Kati). Alijadili neno hili kwa undani zaidi: “Wakati mwingine hadhi hii inatokana na sababu za nje na wakati mwingine inatokana na sababu za ndani. Je, ni sababu ya kifedha, kimwili, kiuchumi? Haiwezi kuwa imesimama peke yake” (Mashariki ya Kati). Alisisitiza umuhimu wa kuzingatia viwango anuai vya kuathirika kwa haraka na kuzingatia utangamano wakati wa kuzungumza juu ya kuathirika kwa haraka badala ya kuianglia dhana hii kwa “mtazamo sawa kwa kila mtu.”

Mhojiwa wa utafiti pia alisema kuwa inasaidia zaidi kutumia utangamano kuelezea sababu zinazosababisha kuathirika kwa haraka (Mashariki ya Kati). Washiriki wachache wa mahojiano walitafakari juu ya ukweli kwamba kuathirika kwa haraka hulingana na muktadha: “Neno kuathirika kwa haraka linaonyesha kuwa mtu hana nguvu na wakati mwingine, kuathirika kwa haraka hutegemea mazingira” (Afrika Mashariki). Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alipendekeza neno mbadala ambalo ni tafsiri katika lugha yake asili, ambayo inalingana na “vikundi ambavyo bado havijastawi” kama kibadala cha kuathirika kwa haraka.

LUGHA NA UTAMBULISHO

Mwongozo wa BLTG juu ya ujumuishaji wa wanawake na wasichana anuwai katika kujitayarisha na kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura (Julai 2019) unashughulikia lugha na utambulisho. Katika hati hiyo tulisisitiza umuhimu wa kuuliza wanawake na wasichana juu ya lugha na maneno wanayopendelea; kujiepusha na vifupisho ambavyo vinaweza kuwafanya watu waonekane kama 'wengine' na kupuuza utu; na kujiepusha na ufafanuzi wenye mwelekeo mmoja wa utambulisho wa mtu.

Lugha inayohusiana na vitambulisho maalum ilitajwa tena katika mazungumzo yetu na washiriki wa BLTG katika maandalizi ya utafiti huu. Mshiriki mmoja wa mahojiano ya utafiti huu aliangazia jinsi kuweka watu katika vikundi fulani "kunarahisisha maisha kwa wafadhili na mawasiliano" lakini alipendekeza kuwa kufanya hivi kunamaanisha tunaweza "kuingia kwenye mtego wa kuiona kwa mwelekeo mmoja" (Mashariki ya Kati).

Kwa jumla, matokeo katika sehemu hii ni finyu kwa sababu wahojiwa hawakujumuisha mashirika maalum yanayofanya kazi na wanawake na wasichana wanaoishi na ulemavu, wanawake wazee au wanawake na wasichana walio na mwelekeo tofauti wa kingono, utambulisho na namna tofauti ya kujitambulisha kijinsia. Hata hivyo, maoni kutoka kwa wahojiwa yanasisitiza tena umuhimu wa kushauriana na vikundi maalum vya jamii, wanaharakati na watendaji maalum ili kuhakikisha kuwa lugha inaakisi kile watu wenye vitambulisho hivyo wanapendelea. Hii inaweza kutokana na kuzingatia muktadha - kinachochukuliwa kama lugha yenye heshima na yenye nguvu - au kwa sababu ya kuzingatia usalama. Mshiriki mmoja wa mahojiano alizungumza kuhusu vile neno kama "wanawake na wasichana" linaweza kuwa la kisiasa, kuhusu jinsi au ikiwa linajumuisha watu wasiothibitisha na waliobadili jinsia (Afrika Mashariki). Washiriki pia walionyesha jinsi mitazamo, imani na kaida zinavyounganishwa na lugha, na umuhimu wa kushughulikia maswala ya ndani zaidi kuliko kuchukulia kwamba mabadiliko ya ghafla ya lugha yatashughulikia ubaguzi au upendeleo.

LUGHA NA KUFUMBA MACHO

Lugha inaweza pia kutumiwa kama chombo au kama namna ya kufumba macho - kwa mfano, kujaribu kuonyesha kwamba kazi inajumuisha au inazingatia mahitaji ya vikundi fulani. Katika utafiti huu, asilimia 69 ya wahojiwa walikubaliana kwa kiasi au sana na kauli hii, *"Katika sekta ya kibinadamu, wakati mwingine mimi huhisi kwamba juhudi zetu za kujumuisha wanawake na wasichana ni ishara tu."* (Karibu asilimia 14 hawakuwa na maoni yoyote, asilimia 14 hawakukubaliana na asilimia 3 walisema hawajui.) Wakati wa mahojiano na majadiliano ya vikundi, washiriki walijadili jinsi maneno ya kawaida kama "wanawake na wasichana" yanaweza kutumiwa katika sekta ya kibinadamu. Washiriki wengi walisisitiza umuhimu wa kuhakikisha "wanawake na wasichana" wanatajwa hasa kwa sababu changamoto na mahitaji yao ni tofauti na ya wanaume na wavulana. Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alitoa maoni juu ya umuhimu wa kutaja wazi wanawake na wasichana ili kuhakikisha wanashiriki.

Washiriki wachache walijadili kuwa kutaja tu "wanawake na wasichana" hakuonyeshi utangamano kati ya kuwa mwanamke au msichana na safu zingine za mamlaka au udhalimu. Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema: "Maneno 'wanawake na wasichana' yanatumiwa na wengi lakini kwangu mimi nadhani ni ya jumla sana… Hata hivyo wanawake na wasichana ni anuai na wana mahitaji tofauti… kwa mfano, wanawake walio na VVU / UKIMWI, wanawake wazee… " (Afrika Mashariki). Mshiriki wa majadiliano ya vikundi alitaja haja ya kufafanua zaidi wasichana hawa ni nani: "Kuna wasichana ambao wako shuleni, kuna wasichana ambao hawako shuleni, kuna wasichana wanaobalehe. Ni muhimu pia kuainisha kwa kina zaidi kwa sababu kufanya hivi kunawezesha hatua tunazochukua na uwekezaji wetu katika vikundi hivi vya watu kuwa mahususi zaidi, kuwalenga zaidi na kuwa na maana kwao" (Afrika Mashariki).

Mshiriki mwingine wa mahojiano alisema: "Inaambatana na dhana ya kujumuisha jinsia... Ni kama huwa inajumuishwa ili kuwafanya wafadhili waridhike na malengo unayofikia. Katika hali halisi wanawake na wasichana ndio wanaonufaika zaidi, lakini pia, kuongeza mwishoni mwa sentensi ni... haizingatii maendeleo kama suala kwa ujumla" (Mashariki ya Kati).

UHUSIANO KATI YA LUGHA, MAMLAKA NA NJIA ZA KUFANYA KAZI

Katika utafiti huu, washiriki waliulizwa watoe maoni kuhusu kauli juu ya safu za mamlaka katika sekta ya kibinadamu:

- Asilimia 63 ya wahojiwa walikubaliana kwa kiasi au sana na kauli hii, "Mashirika mengi ya kibinadamu hufanya kazi na maamuzi kwa njia ambazo zinazingatia safu na zinazotoka juu kuelekea chini." Karibu asilimia 29 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 9 hawakukubaliana.

- Asilimia 57 ya wahojiwa walikubaliana kwa kiasi au sana na kauli hii, "Mashirika mengi ya kibinadamu yanazingatia taasubi ya kiume." Karibu asilimia 20 hawakuwa na maoni yoyote, asilimia 11 hawakukubaliana na asilimia 11 walisema hawajui.

Wakati wote wa majadiliano ya vikundi na mahojiano, washiriki waliangazia jinsi safu za mamlaka katika mashirika ya kibinadamu zinaathiri lugha inayotumiwa. Washiriki wengi walijadili jinsi wahusika tofauti hutumia maneno tofauti, na kuhitaji mashirika ya nchini kujirekebisha. Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alisema: "Baada ya kuwa katika sekta ya kibinadamu, wengi wetu tunaweza kukubali kwamba ikiwa unashughulikia miradi mingi, tunabadilisha mienendo ya lugha kulingana na mshirika unayefanya kazi naye… Wao huendelea kurekebisha na kubadilisha, "Hapana, tumewacha kutumia hili, sasa tunatumia hili," kisha wakati ujao 'Tumeacha kutumia hili, tunatumia hilo lingine... Wakati mwingine mabadiliko haya yanaweza kuzidi" (Afrika Mashariki). Kwa maoni kama hayo, mshiriki mmoja wa mahojiano alisema: "Istilahi hizi zote zilizosawazishwa kimataifa, njia za kimataifa za kufanya kazi, huwa tunatupiwa tu… " (Asia).

Washiriki pia walijadili jinsi mashirika ya kimataifa yanavyoathiri istilahi zinazotumiwa na mashirika ya nchini. Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema, "Mara nyingi huja na maneno ya juu ambayo hayawezi kueleweka na jamii za wenyeji. Wakati mwingine hayawezi hata kutafsiriwa na jamii za wenyeji" (Asia). Alitoa mfano wa neno "nexus," ambalo ni ngumu kutafsiri, na vile vile "jinsia," ambalo katika muktadha wake, wakati mwingine hutafsiri kama ya kiume na ya kike, na kutenga makundi mengine. Mapendekezo yake yalikuwa: "Ni muhimu kwa wahusika wa kimataifa kufikiria juu ya athari za istilahi wanapoleta istilahi nchini, na fikiria juu ya maana ya istilahi hizo kwa wenyeji."

Katika utafiti huu, asilimia 29 ya wahojiwa walikubaliana kwa kiasi au sana na kauli hii, *"Katika shirika langu kuna shinikizo la kutumia maneno fulani kuelezea jamii kwa sababu kufanya hivi kunasaidia kuonyesha hitaji na kupata ufadhili."* (Karibu asilimia 26 hawakuwa na maoni yoyote, asilimia 40 hawakukubaliana kwa kiasi au sana na asilimia 6 walisema hawajui.) Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alizungumzia juu ya safu za mamlaka ambazo zinahitaji watumie istilahi zinazotumiwa na wafadhili: "Tunategemea kabisa matumizi ya lugha ambayo wafadhili hutumia. Tunajaribu kuchagua istilahi mbadala na wao huzikataa au kuzibadilisha. Kwa kuzingatia jambo hili, sisi tuko chini yao. " Alitoa mfano wa jinsi hadhi yao kama shirika hubadilika kulingana na mfadhili: "Wakati mwingine tunaitwa Shirika tu Lisilo la Kiserikali, wakati mwingine tunaitwa shirika la haki za wanawake, wakati mwingine tunaitwa asasi ya kiraia, kulingana na neno ambalo mfadhili ataweza kutumia kuturejelea. Kwa kuzingatia jambo hili, tumeshirikishwa tu na hili ndilo neno linaloelezea uhusiano huu kwa kifupi. Tumeshirikishwa katika kutumia istilahi hii, jambo lililojikita katika itikadi ya kuwa sehemu ya mfumo huu wa kibinadamu" (Mashariki ya Kati).

LUGHA NA MIENENDO BADILIFU YA “NCHINI” NA “KIMATAIFA”

Washiriki walitaja kuwa wafadhili na mashirika ya Umoja wa Mataifa huwa na istilahi maalum, ambayo ni maalum sana na ya kiufundi. Mshiriki mmoja alituma maoni ya maandishi, akielezea: “Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya Kimataifa hutumia akronimi na vifupisho, jambo ambalo linatenga wengine. Ikiwa hauelewi vifupisho hivi, hutaelewa mkutano unaohudhuria, au/na pia utapata wakati mgumu kujaza baadhi ya violezo ambavyo vifupisho hivi vimetumiwa” (Mashariki ya Kati). Washiriki wachache pia walibaini kuwa wakati mwingine lugha tofauti huhitajika kutokana na msimamo wa kisiasa wa wafadhili na kwamba jambo hili linaweza kusababisha changamoto katika kuangazia mambo halisi ambayo wale walio katika hali fulani za kibinadamu wamepitia.

Washiriki wachache walisisitiza umuhimu wa kuwa na uelewa bayana wa istilahi na maana yake: “Tunahitaji kushirikiana na mashirika ya kimataifa katika kujadili maneno hayo ili tukubaliane kuhusu maneno sahihi ya kutumia tunapofanya kazi pamoja, ili tuweze kujumuisha wote. Ikiwa kikundi kimoja kinajiona hakijajumuishwa au kinahisi kuwa lugha inayotumika haifai, kitanyamaza… Kwangu mimi nadhani tunahitaji kukubaliana juu ya lugha tunayotumia, juu ya maneno ya kiufundi au yanayofaa ambayo tutatumia wakati tunafanya kazi pamoja” (Afrika Mashariki).

Katika utafiti huu, wahojiwa waliulizwa kutafakari juu ya neno "shirika la nchini" pamoja na safu za mamlaka kati ya mashirika ya ndani mwa nchi na mashirika ya kimataifa:

- Asilimia 23 ya waliohojiwa walisema kuwa walikuwa na hofu kiasi au sana na neno "shirika la nchini." Karibu asilimia 29 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 49 hawakuwa na wasiwasi wowote.

- Asilimia 80 ya wahojiwa walikubaliana kwa kiasi au sana na kauli hii, "Wakati mwingine, ni kama kwamba mashirika ya kibinadamu ya kimataifa hutagusana na mashirika ya ndani mwa nchi kwa njia zenye safu na zinazotoka juu kuelekea chini." Karibu asilimia 9 hawakuwa na maoni yoyote, asilimia 6 hawakukubaliana, na asilimia 6 walisema hawajui.

- Asilimia 66 ya wahojiwa walikubaliana kwa kiasi au sana na kauli hii, "Utaalamu na maarifa ya nchini mara nyingi hayatambuliwi katika ushirikiano wa mashirika ya kimataifa na ya nchini katika sekta ya kibinadamu." Karibu asilimia 14 hawakuwa na maoni yoyote, asilimia 14 hawakukubaliana kwa kiasi au sana na asilimia 6 walisema hawajui.

- Asilimia 80 ya wahojiwa walikubaliana kwa kiasi au sana na kauli hii, "Ikiwa mashirika ya nchini yangepewa fedha zaidi, sauti zaidi na mamlaka ya kufanya uamuzi, tofauti za mamlaka katika sekta ya kibinadamu zingepungua." Karibu asilimia 11 hawakuwa na maoni yoyote, asilimia 6 hawakukubaliana kwa kiasi au sana na asilimia 3 walisema hawajui.

Katika mahojiano na majadiliano ya vikundi, suala ambalo washiriki walijadili zaidi ni uhusiano kati ya mashirika ya nchini na mashirika ya kimataifa. Katika utafiti huu, asilimia 29 ya wahojiwa walisema kuwa wana wasiwasi kiasi au mwingi kuhusu neno "nchini." Karibu asilimia 31 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 40 hawakuwa na wasiwasi wowote.

Washiriki wa mahojiano pia walijadili maana ya neno "nchini." Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema: "Hii ndio maana - hawana chochote, hawana ujuzi, hawana uwezo, hawana utaalamu… Ni kama wao ndio wanajua na sisi hatujui" (Mashariki ya Kati). Mshiriki mwingine wa mahojiano alitoa maoni: "Hasa mashirika ya kimataifa yanapenda kutumia 'ya nchini' kutofautisha kuwa wana rasilimali na maarifa zaidi, na wanafikia watu wengi zaidi. Wakitaja 'nchini', wanamaanisha mtu anafanya kazi katika eneo dogo zaidi" (Afrika Mashariki). Alipendekeza kauli mbadala kama vile, "Tunashirikiana na [jina la shirika]" na kurejelea kama "mashirika yanayofanya kazi katika eneo hili" (Afrika Mashariki). Mshiriki mwingine wa mahojiano alisema: "Ninapendelea kutumia shirika la kitaifa, na sio shirika la eneo husika/nchini. Neno kitaifa ni bora kwa sababu si kiashiria kuwa neno kimataifa lina hadhi na upendeleo zaidi" (Mashariki ya Kati). Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema kuwa katika muktadha wake, neno 'nchini' linahusishwa na historia ya kikoloni ya nchi hiyo na linamaanisha kitu kisichostahili na halina maana nzuri katika lugha ya mitaani ya nchi hiyo (Afrika Mashariki).

Mshiriki mmoja wa mahojiano alipendekeza kwamba neno "nchini" liliweka baadhi ya mashirika katika hadhi ya chini: "Tulipofanya kazi na [Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Kimataifa], yalituchukuliwa kama mashirika ya nchini. Jambo hilo lilihalalisha sababu yao ya kutulipa pesa kidogo… Ndio maana walikuwa wakituita wenyeji, ili kuhalalisha sababu za kutupatia rasilimali kidogo. Wakati huo huo kwao, ni wa kimataifa, na wana rasilimali na mamlaka yote ya kufanya uamuzi juu yenu. Hivyo ndivyo tulivyokuwa tukijihisi. Na wangehakikisha tumehisi vile. Sauti na maneno waliyotumia yalikufanya ujisikie kuwa hauna maana. Kwa sababu wewe ni mwenyeji, haujui mambo fulani" (Afrika Mashariki).

Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema kuwa "Mashirika ya kimataifa huyaona mashirika madogo kama hayana uwezo, lakini huyategemea ili kupata habari na kuweza kufikia maeneo yasiyoweza kufikika". Ukweli kwamba mashirika haya madogo hayajawakilishwa katika maamuzi, ripoti au machapisho "unaweza kuwa aina ya ubaguzi wa rangi" ambao hufanyika katika muktadha wao (Afrika Mashariki).

Mshiriki mwingine wa mahojiano alitoa maoni juu ya nguvu ambazo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Kimataifa huwa nazo juu ya suala la pesa: "Mashirika haya Yasiyo ya Kiserikali ya Kimataifa huchukuliwa kama wafadhili. Huwa yanachukuliwa kama yenye nguvu zaidi… Huwa yanachukua jukumu la usimamizi wa fedha. Huwa yana uwezo wa kudhibiti fedha na yanaweza kutawala mashirika ya kiraia ya nchini kwa sababu yana pesa. Mashirika haya hukutaka ufanye kile wao wanachotaka" (Asia).

URITHI WA KIKOLONI NA UBAGUZI WA RANGI, ULIOIMARISHWA NA LUGHA YA MISAADA

Kama inavyoshuhudiwa hapo juu, mazungumzo haya yanayohusiana na lugha na mamlaka pia yalisababisha tafakari juu ya urithi wa kikoloni na ubaguzi wa rangi katika sekta ya misaada. Asilimia 31 ya wahojiwa walikubaliana kwa kiasi au sana na kauli hii, *"Ubaguzi wa rangi ni shida katika mazingira ninayofanya kazi."* (Karibu asilimia 11 hawakuwa na maoni yoyote, asilimia 51 hawakukubaliana kwa kiasi au sana na asilimia 6 walisema hawajui.) Asilimia 69 ya wahojiwa walikubaliana kwa kiasi au sana na kauli hii, "*Sekta ya kibinadamu inahitaji kushughulikia safu za mamlaka za kikoloni katika uhusiano wetu na jamii.*" (Karibu asilimia 17 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 14 hawakukubaliana kwa kiasi au sana.) Baadhi ya tafakari hizi, zilizohusiana, sio tu na lugha, bali mambo mengine, zimeangaziwa hapa. Tunapendekeza sehemu hizi ili kuendelea kujifunza na kuendeleza mazungumzo.

Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alitafakari juu ya jukumu la ukoloni katika kuimarisha safu za mamlaka: "Kwetu sisi tunaotoka nchi ambazo zina historia ya kupitia ukoloni, wakati mwingine tunahisi kama bado tuko katika wazo la ukoloni. Wakati mwingine bado tunajiona kuwa tuko chini kuliko watu wengine wanaokuja kutoka Ughaibuni… Wakati mwingine hatujiamini kufanya mazungumzo na kushiriki uzoefu wetu au maarifa yetu, kwa hivyo wakati mwingine tunapokea tu maarifa kutoka Magharibi, kutoka nchi zingine, ni bora kuliko yale tuliyonayo" (Asia). Mshiriki wa mahojiano alisema: "Sasa unaona mashirika mengi ya kimataifa yakitekeleza moja kwa moja. Kwa nini?... Kwa nini unalazimisha ajenda ya kikoloni? Ni njia ya kikoloni ya kushirikiana na jamii. Lazima tukatae mfumo huu wa kikoloni" (Mashariki ya Kati).

Washiriki walijadili jinsi mienendo badilifu ya mamlaka inayosisitizwa na lugha ya "kimataifa" na ya "nchini" huathiri mishahara na tofauti katika mikataba. Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema: "Wana mikataba tofauti ya wenyeji na ya watu wa kimataifa. Ni hali tofauti, mshahara tofauti, upendeleo tofauti. Neno '-a kimataifa' na 'a nchini/ mwenyeji'… huleta ukosefu wa usawa" (Mashariki ya Kati). Mshiriki mmoja wa mahojiano aliibua suala la majadiliano ya mishahara na mashirika ya kimataifa: "Walidhani sisi ni wenyeji na tukiwa wenyeji hatuna changamoto kama zao… hatuhitaji rasilimali kama wanavyozihitaji… Walikuwa wakisema, 'Unajua wewe ni mwenyeji, unaishi hapa." Katika mfano huu, Shirika Lisilo la Kiserikali la eneo husika halikuwa na nafasi kubwa ya mazungumzo: "Ilibidi tukubali kile walichokuwa wanapendekeza. Tulijua kuwa hakukuwa na mengi ambayo hangeweza kubadilisha" (Afrika Mashariki). Mshiriki mwingine wa mahojiano alisema: "Ikiwa wewe ni mwenyeji, lazima ukubali kila kitu bila majadiliano. Unaonekana kama huwezi kujitegemea na kujifanyia uamuzi wako huru" (Mashariki ya Kati).

Lugha, mamlaka na jamii tunazohudumia

Katika utafiti huu, asilimia 77 ya wahojiwa walikubaliana kwa kiasi au sana na kauli hii, "Jamii zitashangaa zikisikia baadi ya maneno tunayotumia kuwaelezea." Karibu asilimia 17 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 6 hawakukubaliana kwa kiasi au sana.

Katika mahojiano na majadiliano ya vikundi, washiriki waliangazia umuhimu wa kuhakikisha maneno yanafaa kwa jamii na yanatafsiriwa kwa usahihi ili kunasa maana halisi. Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema: "Itakuwa vizuri sana ikiwa tunaweza kupata maneno kutoka kwa jamii zetu. Ikiwa tunakuja na maneno yetu wenyewe, jambo hili linaweza kuwafanya watu wahisi kama 'wametengwa'" (Afrika Mashariki).

HATUA ZA KUCHUKUA: KUBUNI LUGHA MPYA

Wakati wa majadiliano ya vikundi, mahojiano na tafiti, washiriki walitafakari kwa upana zaidi juu ya jukumu la lugha katika sekta ya kibinadamu. Mshiriki mmoja wa mahojiano alisema: "Lugha inaweza kutumika kama chombo, inaweza kutumika kama silaha, inaweza kutumika kama ngao. Ni muhimu sana ikiwa tunafanya kazi hii iliyojaa siasa, lugha ni muhimu sana na ni muhimu kuzingatia lugha." (Afrika Mashariki). Mshiriki mwingine wa mahojiano alisisitiza umuhimu wa safari ya kujifunza: "Daima tunajifunza kuhusu istilahi ambazo tunatumia. Wakati mwingine haujui kuwa lugha fulani haiimarishi uwezo" (Afrika Mashariki). Ukweli kuwa, kuwagawanya watu ni namna ya kuonyesha mamlaka, pia ulijadiliwa katika kikao kimoja cha mahojiano (Mashariki ya Kati). Mhojiwa fulani wa utafiti alisema, "Wanadamu wote ni sawa na wanastahili heshima sawa, lakini tunawagawanya kwa kuwataja tukitumia maneno haya" (Asia). Mhojiwa mwingine wa utafiti aligusia suala la lugha ya "vurugu" inayotumiwa na wafanyikazi wa kibinadamu, na pia ukweli kwamba lugha katika sekta ya kibinadamu ni ya kiufundi na ina urasmi kama "lugha ya kibiashara" (Mashariki ya Kati).

> *Lugha ina nguvu. Maneno tunayotumia huwa sehemu ya ufahamu wetu. Tunapoyatumia tena na tena, maneno haya yanakuwa ya kawaida.*
>
> Mhojiwa, Mashariki ya Kati

Washiriki wachache walisema kwamba hawakuwa wamefikiria hapo awali juu ya matumizi ya maneno haya: "Hii ni fursa yangu ya kwanza kuzungumza juu ya maswala haya… Hatuzungumzi juu ya maswala haya. Ni kama ni maneno ya kawaida" (Asia). Walitafakari kuhusu ukweli kwamba ilikuwa muhimu kuwa na mazungumzo haya na kuwa makini juu ya maneno yanayotumika. Wengine walitumia fursa hii kutafakari kwa kina juu ya maneno wanayotumia katika kazi yao: "Wakati nilisoma dodoso, niliona aibu" (Mashariki ya Kati). Mhojiwa mmoja wa utafiti alisema kwamba orodha yote ya maneno "inanifanya nihisi vibaya" (Asia). Mshiriki mwingine wa mahojiano alisema: "Kuna maneno mengi katika sekta ya maendeleo na ya kibinadamu ambayo tunatumia bila kutafakari maana yake kwa kina. Hatujiulizi maana yake kwetu sisi na ikiwa kwa kweli yanapitisha maana ambayo tunalenga" (Afrika Mashariki).

Katika utafiti huu, asilimia 66 ya wahojiwa walikubaliana kwa kiasi au sana na kauli hii, "Sina wasiwasi kuwauliza wenzangu na mashirika tunayoshirikiana ikiwa yatatumia maneno ambayo hayafai au hanadunisha wakati tunazungumza juu ya jamii." (Karibu asilimia 20 hawakuwa na maoni yoyote; asilimia 14 hawakukubaliana kwa kiasi au sana.)

Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alijadili umuhimu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutafakari juu ya lugha wanayotumia ili kuamua ni maneno gani watatumia na ni gani hawatatumia: "Shirika Lisilo la Kiserikali linafaa kuamua kile wanachoweza kutumia na kile wanachoruhusiwa kutumia, bila kulazimika kila wakati kukubali kila kitu wanachoandikiwa. Bila kuwa na mazungumzo kuhusu msimamo wenu kama shirika kwanza, hamwezi kutafakari kuhusu maneno haya na maana yake kwenu" (Mashariki ya Kati). Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi pia alitoa maoni juu ya umuhimu wa kuamua maana ya istilahi: "Tangu mwanzo, unamaanisha nini kwa neno hili na kwa nini unalitumia" (Afrika Mashariki). Washiriki kadhaa walionya dhidi ya kubadilisha maneno tu: "Ni ngumu, ikiwa unataka kulifanya lipendeze kidogo, linapoteza maana yake halisi…" (Mashariki ya Kati).

Mshiriki mmoja wa mahojiano alitoa maoni juu ya umuhimu wa kuuliza jamii zenyewe ni maneno gani yanapaswa kutumiwa: "Nadhani ndilo jambo muhimu zaidi. Tunahitaji kuwa na majadiliano makubwa sasa, kama unavyofanya sasa, lakini sio tu na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, lazima tuende kwa jamii hizi, watu ambao tunarejelea kama "vikundi lengwa," watu ambao tunasema "wametengwa," watu ambao tunarejelea kama 'mkimbizi'… Unapenda kuitwa nini, unapendelea nini, linakuathirije ukilisikia? Kisha tunachukua uamuzi kutoka kwa watu hawa juu ya jinsi ambavyo wangependa kurejelewa" (Mashariki ya Kati).

Katika utafiti huo, asilimia 100 ya wahojiwa walikubaliana kwa kiasi au sana na kauli hii, "Watendaji wa kibinadamu wanapaswa kushauriana na wanawake na wasichana ili kuelewa vile ambavyo wangependa kurejelewa." Karibu asilimia 63 walikubaliana kabisa; asilimia 37 walikubaliana tu.

Wakati wa kikao cha uthibitishaji, washiriki walijadili maana wanayoipata kutokana na neno "ufeministi", na fursa zinazotokana na uchambuzi wa kifeministi za kujenga lugha inayoleta mabadiliko zaidi. Mshiriki mmoja wa mahojiano alizungumzia umuhimu wa ufeministi katika kuzungumzia safu za mamlaka: "Njia za kifeministi pia zinatutwika mzigo wa kutumia uchambuzi wa mamlaka, kujua kwamba hakuna kitu kisicho na athari... Njia za kifeministi zinakusaidia kuchambua upya safu za mamlaka, kujua kuwa kuna safu za mamlaka ambazo tunahitaji kushughulikia, nafasi zina athari fulani. Yote yanayotusaidia katika kuunda na kuarifu na kuchambua upya" (Afrika Mashariki). Washiriki pia walitambua kuwa maneno "mfeministi" au "ufeministi" bado mara nyingi husababisha kero katika mashirika ya kibinadamu. Asilimia 43 ya wahojiwa walikubaliana kwa kiasi au sana na kauli hii, *"Watu wengi katika shirika langu huhisi kero wanaposikia neno 'mfeministi.'"* (Karibu asilimia 11 hawakuwa na maoni yoyote, asilimia 34 hawakukubaliana kwa kiasi au sana na asilimia 11 walisema hawajui.)

MAADILI NA NJIA ZA KUFANYA KAZI

Katika majadiliano ya vikundi na mahojiano, washiriki walijadili maadili na njia za kufanya kazi. Mshiriki mmoja wa majadiliano ya vikundi alizungumza juu ya maneno yenyewe na jinsi yanavyosemwa: "Kupitia uchaguzi wa maneno na uchaguzi wa lugha, huwa tunabuni aina fulani ya miundo ya nguvu. Kwa hivyo, tunaweza pia kuvunja vizuizi hivi kwa njia ile ile, kwa kutumia lugha, lugha stahimilivu na ya kirafiki zaidi. Huu ulikuwa mfano wakati wa kuandika. Lakini pia wakati wa kuzungumza, kuonyeshana fadhili, na kusema mambo kwa njia ya huruma zaidi. Kuna mengi tunayoweza kuboresha" (Mashariki ya Kati).

Katika utafiti huu, wahojiwa pia waliorodhesha maadili ambayo mashirika ya kibinadamu yanapaswa kutumia ili kupunguza safu za mamlaka kati ya vikundi tofauti. Maadili haya yameonyeshwa kwa picha hapa chini. Maadili katika fonti kubwa ni yale yaliyotajwa na wahojiwa wengi.

Mbali na mapendekezo kutoka kwa utafiti, mahojiano, majadiliano ya vikundi na kikao cha uthibitishaji, jedwali lifuatalo lina mambo ya kuzingatia wakati wa kutumia maneno fulani, na vibadala vinavyopendekezwa. Mambo mengi hapa chini yalitoka kwa washiriki, pamoja na matini zilizosomwa na pia wakati wa ukaguzi na ukamilishaji wa ripoti.

NENO MAMBO YA KUZINGATIA NA VIBADALA

Mnufaishwa

Tambua kuwa watu wanaofaidika kutokana na huduma au shughuli hawafai kupokea misaada tu lakini wanapaswa kushirikishwa kikamilifu kama wadau muhimu ambao tunazingatia. Mwenendo huu unahusisha pande zote mbili.

Vibadala: Mshiriki, mdau, jamii, mshirika

Kujenga uwezo

Tambua kuwa uimarishaji wa uwezo unahusisha pande zote wala sio upande mmoja tu.

Tambua kwamba kila mtu ana uwezo.

Vibadala: Kuimarisha uwezo, kugawana uwezo

Walemavu

Tambua kuwa kikundi hiki hakina sifa moja, lakini kwamba watu wenye ulemavu wana vitambulisho vingine kama jinsia, rangi, umri, n.k.

Vibadala: Watu wenye ulemavu, wanawake na wasichana wenye ulemavu

Kufurushwa

Usilitumie likiwa peke yake, lakini litumie pamoja na muktadha wa ufurushwaji.

Kibadala: Mtu aliyeathiriwa

Uwezeshaji

Tambua kuwa uwezeshaji ni mchakato na hautimizwi kwa mafunzo tu. Unahitaji juhudi za jumla katika viwango anuwai ili kukabiliana na sababu msingi za ukosefu wa uwezo.

Shirika la mashinani

Vibadala: Shirika la jamii, shirika asili

LGBTQI, SOGIE, mashoga na wasagaji

Kutafsiri kifupisho hakusaidii sana.

Vibadala: Wanawake walio na utofauti wa kingono, wanawake na wasichana walio na mwelekeo tofauti wa kingono na namna tofauti ya kujieleza na kitambulisha kijinsia

Shirika la nchini

Vibadala: Shirika la kitaifa, asasi ya kiraia, mshirika, mashirika yanayofanya kazi katika eneo hili, shirika la haki za wanawake, shirika linaloongozwa na wanawake

Kutengwa

Usilitumie likiwa peke yake.

Fafanua ni sababu gani zinazofanya kundi hili kutengwa (k.m., ukosefu wa fursa, ukosefu wa nafasi za kufikia rasilimali, kuwa bado hawajafikiwa, n.k.).

Wachache

Vibadala: Watu wa dini nyingine, watu wa makabila mengine

Wanawake wazee

Tambua kuwa watu wana vitambulisho anuwai (k.m., jinsia, rangi, n.k.) na kwamba kuainisha mtu kwa kuzingatia umri tu kunaweza kumdhalilisha.

Vibadala: Wanawake ambao wana umri wa juu / mkubwa

Kushiriki

Tambua kuwa kuna viwango tofauti vya kushiriki, ikianza na kuwakilishwa tu, ambako ni tofauti na kujieleza au kufanya uamuzi.

Vibadala: Ushirikiano, kushirikisha

Mkimbizi

Tambua kwamba neno "mkimbizi" ni la kisiasa, kwa hivyo kulibadilisha kunaweza kuwa na athari kwa vikundi fulani.

Tambua vipengele tofauti vya vitambulisho vya watu na uwaheshimu kama wanadamu-sio tu kama wakimbizi. Vipengele hivi ni pamoja na vitambulisho vingine kama vile jinsia, rangi, umri, n.k.

Vibadala: Mtu anayefaa kuzingatiwa, mtu aliyeathiriwa

(Za) kipato cha chini

Taja kila nchi kwa jina au eneo

Njia mbadala: Nchi zenye uchumi unaoendelea kuimarika, Kaskazini / Kusini

Jadi

Fafanua ni nini hasa kinachochukuliwa kuwa cha jadi.

Tambua ugumu wa miktadha ya kitamaduni na usidhanie tu mambo kuhusu mila bila kuthibitisha.

Vibadala: Rasilimali za eneo husika, jamii ya eneo husika, wadau wa eneo husika, asili

Mwathiriwa

Kibadala: Manusura

Kuathirika kwa haraka

Usilitumie likiwa peke yake.

Fafanua ni nini kinachoweza kufanya kikundi hiki kiathirike kwa haraka (kwa mfano, hali yao ya kifedha, ukosefu wa fursa, jinsia, eneo la mijini / vijijini, n.k.).

Wanawake na wasichana

Bainisha ni wanawake na wasichana wagani, kulingana na mtazamo wa kutangamana (kwa mfano, wasichana wanaoishi na ulemavu, wanawake wanaoishi na VVU / UKIMWI, n.k.).

Kuwa makini na jinsi neno hilo linatumiwa katika muktadha fulani wa kitamaduni (kwa mfano, tofauti kati ya "mwanamke" na "msichana" zinaweza kuhusishwa na hali ya ndoa katika miktadha mingine, kwa hivyo inaweza kufaa zaidi kutumia "wanawake wachanga" badala yake ya "wasichana."

MAPENDEKEZO

Ufuatao ni muhtasari wa mapendekezo muhimu kutoka kwa utafiti, mahojiano, majadiliano ya vikundi na kikao cha uthibitishaji wa mawazo ya kifeministi kutoa lugha mpya inayojumuisha na inayowezesha, na kuendeleza usawa ndani ya ushirikiano wa kifeministi na shughuli za kuzuia na kukabiliana na GBV. Zifuatazo ni hatua ambazo watendaji wa kibinadamu wanapaswa kuchukua.

CHAGUO ZA LUGHA:

- Uliza jamii ni maneno yapi wangependa yatumike kuwaelezea.
- Tambua fursa za wahusika wa eneo husika kuongoza katika kubuni istilahi kulingana na maarifa yao ya muktadha, ukitambua kuwa kufanya hivi kunamaanisha kuwa huenda watendaji wa kimataifa na wafadhili wakahitaji kutafakari juu ya jinsi wanavyotumia mamlaka yao kuathiri istilahi na kutafuta namna ya kushiriki mamlaka yao.
- Tambua kuwa maneno yana maana tofauti kulingana na muktadha na hakuna uwezekano kwamba maneno yatakuwa mwafaka katika miktadha na lugha zote.
- Tambua maneno yanayofaa, yanayoambatana na muktadha ambayo yanaeleweka katika lugha za wenyeji, ambayo yatatumiwa kama vibadala panapohitajika.
- Hakikisha kuwa kubadilisha maneno ili kuyafanya yawe jumuishi na yawafae wenyeji kunafanywa kwa kuchambua na kutambua mamlaka, na sio tu kwa ajili ya kufumba macho.

LUGHA NA MAMLAKA:

- Buni fursa za kushawishi watendaji wengine wa kibinadamu kukuza istilahi inayojumuisha na kuwezesha zaidi kulingana na mapendekezo kutoka kwa jamii na watu wanaoufahamu muktadha.
- Fafanua wazi maana ya maneno muhimu ambayo hutumiwa katika sekta ya kibinadamu, kwa kuzingatia mienendo ya mamlaka inayoambatana na baadhi ya maneno, kutoeleweka kwa lugha fulani ya kiufundi na athari za maneno kama haya kwa vikundi tofauti.
- Tafakari kwa kina na utambue sehemu ambazo ukosefu wa usawa kimamlaka huathiri uhusiano kati ya mashirika ya “nchini” na ya “kimataifa”, na kati ya mashirika ya “nchini” na wafadhili.

LUGHA KATIKA UBIA:

- Anzisha ubia sawa kimakusudi ili ushirikiano usijikite tu katika kutumia mashirika ya “nchini” kama washirika wanaotekeleza, lakini badala yake ushughulikie kwa busara safu za mamlaka kati ya wahusika tofauti katika kila hatua ya ushirikiano.
- Zingatia fadhili na huruma katika kuanzisha na kudumisha ubia na wahusika tofauti wa kibinadamu, huku ukichukua muda na kuwa mwangalifu ili kuhakikisha uhusiano wowote ni wa heshima, unajumuisha, unawezesha na unaongozwa na kanuni ya kugawana mamlaka.